

MA FUNZO

NYENZO

UTAFITI

# HATUA KWA HATUA

2017 • TOLEO LA 101

[learn.tearfund.org](http://learn.tearfund.org)

UTUNZAJI WA MAYATIMA



KATIKA TOLEO HILI

6 Kusaidia familia yatima kustawi

8 Utotoni wangu katika nyumba ya mayatima

16 Kutumia sanaa kama tiba

17 Kukutanisha watoto na familia

18 Wakati neno 'Familia ya Kulea' lina maana mpya

**tearfund**

# HATUA KWA HATUA

## UTUNZAJI WA MAYATIMA

### KATIKA TOLEO HILI

#### VIPENGELE

- 3 Familia kwanza: Njia bora ya kukabiliana na changamoto ya mayatima
- 6 Kusaidia familia za yatima kustawi nchini Zimbabwe
- 10 Kuijandaa kukabiliana na ulimwengu
- 14 Mabadiliko katika makao ya mayatima
- 17 Kuunganisha watoto na familia zao
- 18 Wakati neno 'Familia ya Kulea' lina maana mpya
- 20 Kutetea haki za watoto yatima
- 24 Hakuna mtoto anayeachwa nyuma

#### YA KAWAIDA

- 5 KUJIFUNZA BIBLIA:  
Je! Mungu anachukia Krismasi?
- 8 MAHOJIANO:  
Utotoni wangu katika nyumba ya mayatima
- 23 Jumuiya

#### CHUKUA UTUMIE

- 12 BANGO:  
Uimarishaji familia
- 16 Kutumia sanaa kama tiba kwa watoto yatima na wale wanaoweza kuathirika kwa urahisi

'Mungu huwakalisha wapweke nyumbani' (Zaburi 68: 6). Mstari huu unaohamasisha unadhihirika katika kila sehemu ya toleo hili la jarida la *Hatua kwa Hatua*. Kote katika Biblia tunaona Mungu akionyesha kuwajali mayatima, wajane na wageni – wale ambao huenda wana upweke na wako katika mazingira magumu. Angependa sana wapate upendo na ulinzi wa familia. Ujumbe huu ni muhimu sana katika jamii ya leo.

Utafiti unaonyesha kwamba mahali bora zaidi pa kulelea watoto ni katika mazingira ya familia yenye kujali na kutunza. Toleo hili linaangazia watu binafsi, mashirika na makanisa yanayotia moyo, ambayo yanajitahidi kuwapa watoto yatima na waliopitia mazingira magumu familia zenyne upendo. Nchini Zimbabwe, shirika la ZOE linasaidia makanisa kutunza watoto yatima katika jamii zao (ukurasa wa 6). Huko Uganda, shirika la CRANE liki makini kutoa usaidizi wa kuunganisha watoto na familia zao (ukurasa wa 17). M'lup Russey anabertilisha utunzaji wa yatima huko Cambodia, pamoja na kuwasaidia yatima hawa kuondoka kwenye taasisi kwa urahisi (kurasa za 10-11). Huko Uchina, shirika la Care for Children linachochea familia kuwakaribisha watoto wenye mahitaji mbalimbali nyumba mwao, wakiwemo wengi wenye ulemavu (ukurasa wa 24).

Tunatarajia toleo hili la jarida ya *Hatua kwa Hatua* litawatia moyo wale wenye makao ya kawaida ya mayatima kutafakari njia za kuboresha na kuimashira huduma wanazotoa, na labda hata kuanzisha mipango ya kuimashira familia na jamii (kurasa 14-15).

Utaona kwamba toleo hili la *Hatua kwa Hatua* 101 lina sura mpya! Tumeanzisha sehemu mpya za kawaida, zikiwemo sehemu ya watoto (ukurasa wa 19) na ukurasa wa jamii (ukurasa wa 23). Tungependa kuangazia maoni yako na 'matatizo magumu' yanayokabili, kwa hivyo tafadhali wasiliana nasi.



Zoe

Zoe Murton - Mhariri

Jalada linaonyesha mtoto aliye katika familia ya kulea huko mkoaa wa Chiang Mai, Thailand. Picha: Care for Children



*Imeandikwa na Markus Köker*

# KUWEKA FAMILIA MBELE: NJIA BORA ZAI DI YA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO YA MAYATIMA

*Mara nyingi Biblia huzungumza kuhusu huruma ya Mungu kwa 'yatima' na mapenzi yake ya kuwakalisha wapweke nyumbani (Zaburi 68:6). Familia nzuri ni zile ambazo watoto hulindwa, kupewa malezi bora na mahitaji yao kushughulikiwa. Katika familia zenyé upendo, watoto hupata ujuzi muhimu maishani na huhisi kuwa wamekubaliwa. Kukua na kuishi bila familia huongeza pakubwa uwezekano wetu kuathiriwa na hatari.*

*Kwa mujibu wa Mapatano ya Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Watoto:*

*'Ili mtoto aweze kukua kikamilifu na kwa njia nzuri, anafaa kukulia katika mazingira ya familia, yenye furaha, upendo na uelewa.'*

## JE, YATIMA NI NANI?

Kwa mujibu wa shirika la Unicef, yatima ni mtoto ambaye mzazi wake mmoja au wote wawili wamefariki. Kulingana na shirika hili, inakadiriwa kuwa kuna mayatima milioni 140 duniani kote. Hata hivyo, takwimu hizi hazionyesi picha kamili ya tazito hili kwani hazijumuishi kundi la 'watoto walio telekezwa' (social orphans). Kundi hili linajumuisha watoto na vijana ambao hawana uhusiano wowote mzuri na familia zao. Watoto walio telekezwa ni kama wale wasio na makazi au mtu wa kuwatunza (chokoraa), watoto wanaoishi kwenye makao ya mayatima au wale ambao wametenganishwa na familia zao kuititia biashara haramu ya usafirishaji binadamu, vita au mambo mengine.

Ukweli ni kwamba, mamilioni ya watoto wanaosemekana kuwa yatima wana mzazi mmoja, nyanya au babu au wanafamilia wengine walio hai. Kulingana na shirika la Save the Children, angalau asilimia 80 ya watoto wanaoishi katika makao ya mayatima wangali wana angalau mzazi mmoja aliye hai.

## MAKAO YA MAYATIMA NA UMASKINI

Mara nyingi, taasisi zinazowatunza watoto yatima (ikiwa ni pamoja na makao ya mayatima) huonekana kama suluhisho la changamoto hii ya watoto yatima na huenda zilianzishwa kwa nia nzuri. Hata hivyo, baadhi ya nyumba hizi huchukuliwa kama biashara ambapo watoto huonekana kama njia ya kuleta mapato. Kutokana na sababu hii, kumekuwa na visa vya biashara haramu ya kuwasafirisha watoto hadi nyumba kama hizi.

Katika nchi zinazoendelea kustawi, mara nyingi umaskini ndiyo sababu kuu ambayo hufanya watoto wapelekwe kwenye makao ya mayatima. Huenda wazazi au wanafamilia wengine wakaamini kuwa makao haya ya mayatima yatawapa watoto wao chakula, malazi na elimu, mambo ambayo wao watashindwa kuwapa. Kutokana na sababu hizi, ambazo huitwa 'pull factors', idadi ya watoto katika makao ya mayatima huongezeka na kufikia viwango ambavyo vyawenza kuepukika. Kwa mfano, ingawa idadi ya watoto wanaoweza kuathirika kwa urahisi nchini Cambodia imepungua, idadi ya makao ya mayatima iliongezeka kwa asilimia 75 kati ya 2005 na 2010. Hata hivyo hakuna makao ya mayatima yanayoweza kuwatunza na kuwalinda watoto kama inavyofanya familia yenye upendo.

## KUELEWA ATHARI HASI

Utafiti umeonyesha kuwa, kuwatunza watoto kwa muda mrefu katika makao haya ya mayatima hakuwasaidii. Badala yake, maisha yao yanaweza yakaathirika kwa njia mbalimbali zikiwemo:

- **Kuchelewa kukua kisaikolojia na kijamii:** Watoto huwa hawatunzwi na kuangaliwa kama wanavyohitaji. Hivyo, huenda wasiwe na ujuzi wa kiakili, kimwili, kijamii na kihisya wanaohitaji katika umri wao. Pia, huenda



Familia thabit na yenye upendo ndipo mahali pazuri zaidi pa kuwalelea watoto. Picha Marcus Perkins/Tearfund

wasipate ujuzi wanaohitaji ili waweze kujitegemea kimaisha hapo baadaye.

- **Kushindwa kuwa na uhusiano thabiti na wengine:** Wakati watoto hawa wanapokua, huwa wanatagusana na wafanyakazi, watu wakujitoa na wageni tofauti. Kwa sababu hii, huwa hawajengi uhusiano thabiti na wa kudumu kama inavyohitajika.

- **Kuwategemea wengine:** Katika taasisi, kila mara huwa kuna mtu aliye na jukumu la kukimu mahitaji msingi ya watoto na kufanya uamuzi kwa niaba yao. Kwa kawaida, watoto huwa hawapewi nafasi ya kuwajibika katika msingi wa kuaminiana. Jambo hili hufanya iwe vigumu kwa watoto hawa kujitegemea wanapokuwa watu wazima.

- **Usafirishaji haramu na kudhulumiwa:** Tasisi nyingi hazina sera za kuwalinda watoto na huenda zisichunguze historia ya wageni na wafanyakazi wanaofika pale. Jambo hili huwaweka watoto wengi katika hatari ya kuibwa na kudhulumiwa kimwili na kimapenzi.

- **Kutengwa na jamii:** Kwa kawaida, watoto wanaoishi katika makao ya watoto huwa wametengwa na familia na jamii. Mara nyingi wanapotoka kwenye nyumba hizi, huwa wanatatizika kujiunga tena na jamii.

Vijana wengi wanapotoka kwenye makao ya mayatima, huwa wanawenza kuathirika kwa urahisi na nyingi za taasisi hizi za kuwatunza huwa hazina mikakati ya kuwaongoza vijana hawa katika utaratibu huu. Utafiti uliofanywa kwa muda mrefu nchini Urusi ulionyesha kuwa mmoja kati ya watoto watano yatima wanaotoka kwenye makao haya ya mayatima huwa wanajiusisha na uhalifu, mmoja kati ya watoto saba huwa wanaingia kwenye ukahaba na mmoja kati ya watoto kumi

## MANENO YALIYOTUMIWA KATIKA TOLEO HILI

Ulezzi mbadala ni wakati ambapo mtu mwininge kando na wazazi halisi anamtuunza mtoto, k.m. kutunzwa na wanafamilia, familia ya kulea, wazazi wa kuasili au utunzaji wa watoto katika makao ya mayatima.

Utunzaji wa watoto katika makao ya mayatima unamaanisha kumtunza mtoto nje ya misingi ya familia.

**Kubadilisha mkakati** kunarejelea mababiliko ambapo makao ya mayatima huwachana na jukumu la kuwatunza watoto wao wenyewe na badala yake kuwasaidia watoto hao kupata familia na jamii zitakazowatunza.

huwa wanajiuu (Judith Harwin, *Children of the Russian state 1917–1995*).

### NJIA BORA ZAIDI

Habari njema ni kuwa, kote duniani watu wameanza kutambua kwamba kuna njia bora zaidi za kuwatunza watoto yatima na wanaoweza kuathirika kwa urahisi. Baadhi ya njia hizi ni kama:

- **Kuimarishe familia:** Tunaweza kuimarishe na kusaidia familia ili zisiwapeleke watoto kwenye makao ya mayatima. Baadhi ya njia za kuwasaidia ni kuwapa mafunzo ya malezi, ulinzi wa kutwa na shughuli zinazowawezesha kujikimu kimaisha. Ni muhimu kuwasaidia wazazi kujua kwamba familia ni ya kudumu na kwamba wanaweza kufanya kazi bora zaidi ya malezi kuliko makao ya mayatima.

- **Kuunganisha watoto na familia zao halisi:** Chaguo bora zaidi ni kuwaunganisha watoto walio katika makao ya mayatima na familia zao, ikiwa ni jambo ambalo lawezekana na salama. Hatua hii huhushisha kujaribu kuyatatua matatizo yaliyowafanya watengane na familia zao, ikiwa yawezekana.

- **Kutunzwa na wanafamilia wengine:** Ikiwa haiwezekani kuwaunganisha watoto na familia zao halisi, wanaweza kuunganishwa na wanafamilia wengine. Mayatima wengi huwa na wanafamilia wengine ambao watakubali kuwatunza, iwe ni shangazi, wajomba, nyanya au babu, wakubwa wao au mwanafamilia ye yeyote mwininge. Mara nyingi inawezekana kuwafutu na kuwapata wanafamilia hawa na kuwasaidia kumtunza mtoto husika.

- **Familia za kulea:** Kuna familia ambazo huwa tayari kumtunza mtoto ambaye si wao. Wakati familia ya mtoto husika inatafutwa, yeye anaweza kutafutiwa familia nyingine ya kumlea. Pia anaweza, kama suluhisho la kudumu, kuwekwa moja kwa moja chini ya utunzaji wa familia ya kulea. Katika baadhi ya nchi, njia hii hutumiwa kumpatia mtoto familia ya kumtunza daima.

- **Kuasili watoto:** Wakati haiwezekani kuwaunganisha watoto na familia au jamaa zao, wao wanaweza kutunzwa na wazazi waliowaasili. Katika chaguo hili, wazazi hukubali kisheria kumtunza daima mtoto ambaye hawajamzaa. Ni rahisi kwa mtoto anapotoka katika nchi sawa na familia inayomwasili. Kuasili mtoto kutoka nchi tofauti huwa na matatizo mengi. Hivyo, Mapatano ya Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Watoto hupendelea mtoto anapoasiliwa na familia inayoishi katika nchi sawa na mtoto husika.

- Wakati mwininge kuna haja ya kumpeleka mtoto kwenye makao ya **mayatima** (kwa mfano, mtoto aliyeipitia mazingira magumu, wakati masuluhihi mengine yanatafutwa). Lakini katika hali nyingi, hili linafaa kuchukuliwa kama chaguo la mwisho na lisilo la kudumu. Iwapo ni lazima mtoto apelekwe katika makao ya mayatima, lazima mazingira yafanane na yale ya familia kadri iwezekanavyo, yaani awekwe katika nyumba isiyo na watoto wengi badala ya kuwekwa kwenye nyumba yenye watoto wengi.

Walio na jukumu la kumtunza mtoto husika wanafaa kuitia chaguo walizo nazo za ulezzi mbadala ili waone chaguo linalomfaa zaidi.

### SERA ZA KITAIFA ZINABADILIKI

Nchi nyingi sasa zinatekeleza chaguo hizi za ulezzi mbadala na kuzifanya sera zao rasmi. Kwa mfano, katika mwaka wa 2012, nchi ya Cambodia ilitangaza sera mpya iliyolenga kuwaweka watoto chini ya ulinzi wa familia badala ya makao ya mayatima. Kando na kuwafaa watoto, chaguo hili haligharimu pesa nyingi. Kwa mfano, katika nchi ya Uganda, utafiti ulionyesha kuwa makao ya mayatima yanaghari mu pesa mara 14 zaidi ya gharama ya kumtunza mtoto katika jamii (Unicef).

### JE, TUNAWEZA KUFANYA NINI?

Kanisa linaweza kuchangia pakubwa katika kubadilisha jinsi tunavyowatunza mayatima na watoto walipitia mazingira magumu. Vuguvugu la The World Without Orphans limewaunganisha wakristo, makanisa na

mashirika duniani kote kufanya kazi kwa pamoja ili kuwapa watoto utunzaji wa familia. Vuguvugu hili ambalo lilianza nchini Ukraine limeanzisha miradi ya kitaifa katika zaidi ya nchi 26. Kutokana na kazi yake, idadi ya watoto wanaoasiliwa na kuwekwa chini ya ulezzi wa familia zinazoishi katika nchi husika imeongezeka.

Kuna baadhi ya mambo ambayo watu binafsi, makanisa na mashirika yanaweza kufanya ili kuboresha utunzaji wa mayatima. **Watu** wanaweza kujitelea kuwa wazazi wa kuasili au kulea, na kuwashimiza wengine kufanya hivyo. **Makanisa** yanaweza kuanzisha programu za kuimarisha familia na kuwasaidia mayatima katika makanisa na jamii. **Wasimamizi** wa vituo nya kuwatunza watoto wanaweza kutafuta njia za kubadilisha mkakati wanaotumia sasa na kuanza kutoa huduma za kuimarisha familia na jamii kwa jumla. Sote tunaweza kuhimiza serikali zetu zitekeleze sera zinazopatia utunzaji katika familia kipaumbele. Kwa kushirikiana na wengine walio na maono sawa, tunaweza kujaribu kumpatia kila mtoto nafasi ya kuishi katika familia yenye upendo.

.....

Markus Köker ndiye Msimamizi wa Miradi ya Kimataifa katika shirika la Tearfund Ireland.

Tovuti: [www.tearfund.ie](http://www.tearfund.ie)

Barua pepe: [enquiries@tearfundireland.ie](mailto:enquiries@tearfundireland.ie)

**World Without Orphans**

Tovuti: [www.worldwithoutorphans.org](http://www.worldwithoutorphans.org)

Barua pepe: [info@worldwithoutorphans.org](mailto:info@worldwithoutorphans.org)



► Katika nchi zinazoendelea kustawi, umaskini ndiyo sababu ambayo mara nyingi inafanya familia ziwapeleke watoto katika makao ya mayatima.



*Imeandikwa na Krish Kandiah*



# KUSOMA BIBLIA

## JE, MUNGU ANAICHUKIA SHEREHE YA KRISMASI?

*Je, waweza kuhisi aje iwapo nitakwambia kwamba Mungu anachukia Krismasi? Au kwamba anachukizwa na sherehe za Noeli, Kwaresima na Pasaka? Je, na nikikwambia kwamba mikutano ya maombi humchosha na ushirika humkera?*

### *Kweli?*

Hivyo ndivyo inaonekana Mungu yuasema katika mojawapo ya vifungu vya Biblia vinavyoniogopesha sana:

*'Msilete tena matoleo ya ubatili; uvumba ni chukizo kwangu; mwezi mpya wa sabato, kuita makutano; siyaweki maovu hayo na makutano ya ibada. Sikukuu zenu za mwezi mpya na karamu zenu zilizoamrishwa, nafsi yangu yazichukia; Mambo hayo yanilemea; nimechoka kuyachukua. Nanyi mkunjuapo mikono yenu, nitaficha macho yangu nisiwaone; Naam, mwombapo maombi mengi, sitasikia; Mikono yenu imejaa damu.'* (Isaya 1:13-15)

Je, Mungu kwa kweli anawaambia watu wake wasitishe ibada zao? Je, kwa kweli anasema kuwa maombi hayana maana?

Si eti Mungu anapinga sadaka: ni yeye aliyeamuru zitolewe. Si eti Mungu hataki maombi: ni yeye aliyeanza kunena nasi. Si eti Mungu hafurahii sherehe: ni yeye aliyezanzisha.

Hakuna lolote kati ya haya ambalo limejikita katika kuabudu. Mungu amerahisisha mambo katika vifungu vifuuatavyo (Isaya 1:16-17), ambapo yeye anaeleza kwa sentensi sita fupi ibada ya kweli:

1. **Acheni kutenda mabaya.**
2. **Jifunzeni kutenda mema.**
3. **Takeni hukumu ya haki.**
4. **Wasaidieni walioonewa.**
5. **Mpatieni yatima haki yake.**
6. **Mteteeni mjane.**

Hii ndiyo aina ya ibada ambayo Mungu anahitaji kutoke kwa watu wake. Ingekuwa vyema kwa Mungu kama tungekomesha ibada zetu badala ya kuendelea nazo huku tukitelekeza mambo haya sita.

Kanisa nyingi hufanya kazi nzuri ya kufunza jambo la kwanza, 'Acheni kutenda mabaya.' Pia baadhi ya kanisa zinafunza vizuri jambo la pili, 'Jifunzeni kutenda mema.' Lakini mara nyingi, mambo hayo mengine, nambari tatu hadi sita, huwa hayafunzwi.

Mwenyewe ningependelea kanisa ligundue aina hii ya ibada kwa kushughulikia jambo la tano, 'Mpatieni yatima haki yake.' Tunaishi katika ulimwengu wenye dosari, ambapo kuna mamilioni ya mayatima. Baadhi ya watoto hawa wamo katika jamii zetu. Lakini wakristo na makanisa yanaanza kugundua kina cha ibada ya kweli kinachofikiwa tunapoanza kumtii Mungu na kuwapatia mayatima haki zao. Katika kazi yangu hapa Home for Good, huwa ninasikia visa vingi vya wakristo wanaowapatia makazi watoto

waliopitia mazingira magumu. Wanaofanya hivyo hupata kwamba wao wenyewe ndio wanaobarikiwa na kubadilishwa upya.

Nchi nyingi kote duniani zimeanza kutambua kwamba mahali bora zaidi pa watoto waliopitia mazingira magumu kustawi si katika makao ya mayatima, bali ni katika familia. Tunajua kwamba Mungu 'huwakalisha wapweke nyumbani' (Zaburi 68:6) na kwamba 'Dini iliyo safi, isiyo na taka mbele ya Mungu Baba ni hii, Kwenda kuwatazama yatima na wajane katika dhiki yao' (Waraka wa Yakobo 1:27). Ibada ya familia hupata maana mpya tunapowafungulia nyumba zetu watu waliopitia mazingira magumu kutoptana na neema na mapenzi ya Mungu maishani mwetu.

Kwa kweli Mungu hachukii Krismasi. Tuisihau kwamba katika hadithi ya Krismasi, Mungu huonyesha upendo wake kama Baba kwa ulimwengu. Anawapatia Maria na Yusufu jukumi la kumlea mwanawie ili afungue njia ya sisi kuingia katika familia yake. Tumpatие Mungu ibada ambayo inaambatana na matakwa ya injili yetu. Hebu tungundue maana ya kumpatia yatima haki yake.

*Dr. Krish Kandiah ndiye mwenyekiti wa paneli ya theolojia ya Tearfund. Yeye ni mzazi wa kulea na kuasili. Krish alianzilisha shirika la Home for Good, ambalo huwatafutia watoto wenye haja familia za kuwalea na kuwaasili nchini Uingereza.*

*Tovuti: [www.homeforgood.org.uk](http://www.homeforgood.org.uk)  
Barua pepe: [info@homeforgood.org.uk](mailto:info@homeforgood.org.uk)*

*Imeandikwa na Denford Munemo na Qobolwakhe Khumalo*

# KUSAIDIA FAMILIA ZA YATIMA KUSTAWI NCHINI ZIMBABWE

*Nchini Zimbabwe kuna takriban watoto yatima 720,000, sababu mojawapo ikiwa vifo kutokana na magonjwa yanayohusiana na UKIMWI. Kwa kawaida, familia na jamaa wengine walichukua jukumu la kuwatunza watoto yatima. Hata hivyo, hali ngumu ya kiuchumi na kijamii nchini imewaacha jamaa wakitatizika. Shirika la ZOE (Zimbabwe Orphans through Extended Hands) linaamini kwamba makanisa yaliyo karibu yana jukumu muhimu katika suala hili.*

## KUHAMASISHA MAKANISA

Kuhamasisha makanisa ni nguzo msingi katika kazi ya shirika la ZOE. Mara nydingi makanisa huwa na hamu ya kutunza yatima, lakini hawajui la kufanya. Shirika la ZOE hujia hapa.

Nguvu ya huduma hutokana na makanisa kufanya kazi pamoja. Kiongozi wa kanisa akienda kwa shirika la ZOE kutafuta msaada na kutunza yatima, shirika hili kwanza humwombia mchungaji akusanye viongozi wote wa kanisa katika eneo hilo. Kisha wafanyakazi wa ZOE huwapa viongozi wote pamoja ujumbe kutoka kwa Biblia wa kutunza yatima. Viongozi hawa hurudi

kwenye makanisa yao na kushiriki ujumbe huu ama maono haya. Kisha wao huwaomba washirika ambao wangependa kuwatunza yatima wajitolee.

Baada ya hapo ZOE huwafundisha waliojitlea kutembelea na kusaidia familia za yatima (familia ambazo zinatunza watoto yatima). Kila aliyejitlea huwa na jukumu la kutembelea familia nne au tano za watoto yatima mara kwa mara (idadi hii ya mara huwa chache ikiwa familia inaoongozwa na mtoto, kwani familia hizi zinahitaji msaada zaidi).

## KUIMARISHA FAMILIA

Washiriki waliojitlea hupewa mafunzo ya malezi, kuandaaj bajeeti, ulinzi wa watoto, jinsi ya kutoa usaidizi wa kisaikolojia na kijamii, ukuaji wa watoto na masomo ya masuala ya ngono na uzazi. Nao hushiriki maarifa haya na familia wanazosaidia.

Makanisa na wanajamii pia huhimizwa kutetea mayatima. Wao hulinda haki za urithi za familia yatima na kuwasaidia mayatima wapate yeti vya kuzaliwa, ambavyo wanahitaji ili kupata huduma zingine.



ZOE hupatia familia yatima nafasi za kujikumu maishani, na washiriki wa kanisa wanaojitlea hutoa msaada. Picha : Eleanor Bentall/Tearfund

Ujenzi wa mahusiano ya kusadiana ni muhimu katika jukumu la waliojitlea. Kama sehemu ya mafunzo wanayopata, wao huhimizwa watumie rasilimali walizopewa na Mungu kusaidia familia za yatima (tazama ukurasa unaoangaliana na huu).

## UCHUMAJI RIZIKI WA KUDUMU

Shirika la ZOE pia husaidia yatima na walezi wao kupata njia za kuchuma riziki. Wao huwapa mifugo kadhaa (mfano mbuzi, kuku au sungura) na kufundisha wanafamilia jinsi ya kuwachunga wanyama hao. Wao pia hufundisha familia za yatima kukuza mazao na kuwapa yatima mafunzo ya ujuzi ya aina wanayojichagulia, hivyo kuwasaidia kuwa na mustakabali imara zaidi.

.....

*Denford Munemo ni Mkurugenzi wa Taifa wa ZOE, na Qobolwakhe Khumalo ni Msimamizi wa Mipango ya ZOE.*

Tovuti: [www.zoezim.blogspot.co.uk](http://www.zoezim.blogspot.co.uk)  
Barua pepe: [info@zoezim.org](mailto:info@zoezim.org)



## KUREJESHA MATUMAINI KATIKA MAISHA YALIYOPOTEZA MAANA

*Mchungaji Bob Chimboo kutoka Zimbabwe kusini-mashariki anatusimulia jinsi hali imekuwa wakati anafanya kazi na ZOE.*

Kupitia usaidizi wa ZOE, tulianzisha miradi ya kutunza yatima katika kanisa 135 huko Masvingo kati ya 2003 na 2016. Maisha ya wengi waliokuwa wamepoteza matumaini 'yamepata matumaini'. Makanisa yametambua njia nydingi za kukidhi mahitaji ya yatima na wajane. Baadhi ya njia hizi ni kulipa karo ya shule na kufundisha ujuzi wa kutengeneza nywele, ufundi wa mitambo ya magari na kushona. Baadhi ya yatima hawa sasa

wana kazi na wanaweza kuchumia familia zao riziki. Tunazipa familia yatima mafunzo katika ukulima bustani, kilimo cha samaki, utengenezaji mishumaa, ufugaji mbuzi na kutengeneza siagi ya karanga. Pia tumekuwa tukipinga ndoa za watoto na aina zote za unyanyasaji wa watoto.

Mfumo wa ZOE umetusaidia sisi kama wachungaji kutoka makanisa tofauti kuungana ili kuwasaidia yatima. Huwa tunakutana mara moja kwa mwezi ili kujadili masuala ambayo washiriki waliojitlea kutoka makanisa yetu wamekumbana nayo wakati wa ziara zao. Sasa sisi ni kanisa lenye maana katika jamii zetu.

# KUTUMIA RASILIMALI ULIZOPEWA NA MUNGU

*Wafanyakazi wa ZOE hutumia mawazo haya chochezi kama sehemu ya mafunzo wanayotoa kwa washiriki kanisani waliojitlea. Unaweza kutoa nakala ya kijitabu hiki na uitumia kanisani mwako*

Mungu alituumba tukiwa na moyo, macho, masikio, mdomo, mikono na miguu. Waliojitlea kutoka kanisani wanaweza kutumia rasilimali hizi tulizopewa na Mungu kujenga mahusiano kwa nia ya kusaidia familia yatima.

## MASIKIO


Kusikiliza watoto na kuelewa uchungu wao ... Kumsikiliza babu ambaye sasa anajukumu la kuchunga watoto sita na anajua ana wanne zaidi njiani mtoto wake wa pili akifa ... Kusikiliza wakati hakuna jamaa ye yeyote aliyeuliza: 'Je, waendeleaje?' au 'Watoto wako aje?' Lakini sasa mtu huyu aliyejitlea amekuja kutembelea, na anauliza: 'Unachunga watoto wangapi? Wanaendelea vipi? Habari yako?' Mtu huyu aliyejitlea anasema angetaka kusaidia kwa njia yoyote anayoweza, na anampa mtu huyo nafasi ya kuzungumza kwa mara ya kwanza baada ya miezi mingi. Kisha mtu huyu aliyejitlea anauliza kama anaweza kurudi – na anarudi!

## MIKONO

Kwa msaada wa vitendo, kama vile kuezeka nyumba kwa makuti, kuandaa mashamba kwa ajili ya kupanda, kufundisha kushona au useremala nk.

## MIGUU

Kupeleka ujumbe, kuleta vifaa vinavyohitajika, kupeleka watoto kliniki nk – pamoja na kucheza spoti na michezo!



## MACHO

Kuona nywele za rangi nyeusi na mikono na miguu iliyovimba inayoashiria maradhi ya utapiamlo kutokana na ukosefu wa protini na virutubisho vingine (kwashiorkor) ... Kuangalia macho ya mtoto na kuona 'unyanyasaji' ... Kuangalia nyumba – shimo kwenye paa, ukosefu wa sufuria na vifaa vingine nk ...

## MDOMO

Kuwapa wengine ujumbe wa matumaini kutoka kwa Biblia na ushauri wenyewe hekima. Kuzijulisha familia msaada na huduma zinazopatikana katika jumuiya. Kusema bila woga kwa niaba ya wasiweza kujisemea kupitia utetezi.

## MOYO

Moyo ulioja upendo kwa sababu ya msalaba wa Yesu. Moyo kama Mungu Baba, wa kupenda na kutunza yatima.

Mungu ametupa uwezo huu wa kuwatanza wengine na kuonyesha upendo wa Yesu. Uwezo huu wote ametupa bure! Washiriki wa kanisa wanaweza kutumia rasilimali hizi kuanza kujenga huduma imara ya kutunza yatima.

Mfano: Lloyd Kinsley / Tearfund

# MAHOJIANO

## UTOTO WANGU KATIKA NYUMBA YA WATOTO

*Mamake Peter Kamau Muthui alikuwa akiba na umri wa wiki sita, na babake akafa mwaka mmoja baadaye. Yeye na ndugu zake watano wakubwa walikulia katika makao ya watoto nchini Kenya. Hapa anatueleza jinsi jambo hili liliathiri maisha yake na jinsi liliviyomfanya aanze shirika la Child in Family Focus – Kenya.*

Hali ilikuwaje kwako kukulia katika nyumba ya watoto?

Mimi kukulia katika nyumba ya watoto kulikuwa na uzuri wake na ubaya wake. Nilifurahia safari za mara kwa mara ili kuona ulimwengu nye ya nyumba hiyo, hasa nilifurahia kwenda shulenii na kanisani. Nakumbuka vizuri sana mara yangu ya kwanza kusherekea siku yangu ya kuzaliwa, nilikuwa na umri wa miaka saba. Mwalimu wangu wa shule ya chekechea, Mercy, aliniandalia keki kubwa na akaileta shulenii. Nilisherekea tena siku yangu ya kuzaliwa nilipofikisha miaka 20.

Nilikuwa mmoja wa watoto 30 waliotunzwa na mama wawili wa nyumba, ambao walifanya kazi kwa kubadilishana. Hivyo, ilikuwa vigumu kwangu kuangaliwa, kupewa upendo, utunzaji na uongozi niliohitaji ili kuwa na maisha yaliyofaa na yenye furaha ya utotoni. Mahitaji yote ya kimwili tulipata. Ila hatukuwa na upendo na mapenzi.

Nilizoea kufuata taratibu na nikaona matokeo makali ya kutozifua. Kupata wa kukusaidia kukamilisha kazi ya shulenii ilikuwa changamoto. Haikuwa rahisi kwa mama wa nyumba kutenga dakika tatu kukusaidia kutatta swalii ngumu la hesabu.

Nilipoona watoto wengine, ikiwemo marafiki zangu, wakipata familia za kuwalea au kuwaasili, nilijuliza wakati wangu utafika lini. Kila wakati wagoni wapotutembelea kwenye nyumba hiyo ya watoto, nilihakikisha nimeonesha nidhami ya hali ya juu. Nilitaka kuongeza nafasi zangu za kupendwa na kuchukuliwa kuwa sehemu ya familia.

Mwanzoni, ndugu zangu wanen walikuwa katika taasisi tofauti na mimi na dada yangu mdogo. Hatimaye tuliharnishwa na kupelekwa kwenye nyumba sawa ya watoto. Nilitamani kuona ndugu zangu wakubwa, lakini hili liliwezekana tu katika hafla maalum na wakati mwingine wakati wa kupata mlo.

Bado ninahisi athari za ushirikiano huu finyu na ndugu zangu wakubwa. Hatuna uhusiano wa karibu. Tukio la ndugu yangu mkubwa kujitoa uhai katika mwaka wa 2007 liliathiri familia pakubwa. Linaonesha kwamba vijana wengi wanaondoka kwenye makao ya watoto huwa wanakabiliwa na mfadhaiko na mawazo ya kujiua.

Licha ya changamoto za kulelewa kwangu, nashukuru nyumba ya watoto kwa kunifanya jinsi nilivyo leo. Ninaamini kabisa kwamba Mungu aliniruhusu nipitie hayo akiwa na sababu fulani. Yaliniandaa kuwa mtetezi wa mabadiliko.

### MUNGU HALETI UCHUNGU BILA SABABU, BADALA YAKE YEYE KUFANYA UCHUNGU HUO KUWA CHANZO CHA UZURI NA NIA

**Je! Ulijihisi tayari kukabiliana na ulimwengu wa nje wakati wa kuondoka kwenye nyumba ya watoto?**

Hapana, sikuwa tayari kukabiliana na maisha kwa nje ya nyumba. Kama wengi waliokuwa wameondoka mbele yangu, niliachwa kujisimamia peke yake.

Kwa miaka mingi nilitegemea utaratibu fulani ambapo sikuwa na chaguo lolote au nilikuwa



Peter Kamau Muthui ndiye mwanzilishi wa shirika la Child in Family Focus – Kenya.

na chaguo finyu. Kwa hivyo, nilisumbuka sana na maisha ya kujitegemea. Kuwa na mahusiano na watu, kupika na kuandaa bajeti zilikuwa changamoto kwangu.

Kwa sababu ya kutokuwa na uhusiano mzuri na watu wazima katika nyumba ya watoto, sikujiamini na nilikosa ujuzi msingi wa kushirikiana na jamii. Changamoto hii ilijumuisha ujuzi niliohitaji katika kuanzisha familia.

Licha ya haya, nadhani 'hali haikuwa ngumu sana kwangu'. Muda mfupi baada ya kumaliza masomo yangu ya chuo, nilipewa nafasi ya kufanya kazi katika nyumba hiyo ya watoto. Mwanzoni nilikuwa msaidizi wa mwalimu. Kisha nikawa msaidizi wa mfanyakazi wa kijamii wakati nilipokuwa nasomea shahada yangu ya kwanza. Baadaye nilifanya kazi kama Msimamizi wa Mipango inayohusu Jamii kwa miaka tisa.

**Ulipata ujuzi upi katika wadhifa wako wa Msimamizi wa Mipango inayohusu Jamii katika nyumba hiyo ya watoto?**

Kwanza, nilijifunza kwamba kuwa yatima si sababu kuu inayowafanya watoto kupelekwa katika makao ya watoto. Wengi wa watoto katika nyumba hiyo walikuwa na mzazi mmoja au wote wawili hai, pamoja na jamaa wengi wenye uwezo. Sababu kuu ya kuwapeleka watoto katika nyumba hiyo ilikuwa umaskini. Watu walidhani kuwa utunzaji katika makazi hayo ulikuwa bora zaidi ya kuishi na jamaa.

Pili, nilijifunza kwamba hata utunzaji wa taasisi za ubora wa juu hauwezi kuchukua nafasi ya familia! Familia huwapa watoto upendo na kuwafanya wajihisi wanastahili. Familia huwafunza watoto jinsi ya kuhusiana katika jamii na kuwasaidia kuungana na jumuiya pana. Watoto 'hutimiza umri ambapo' wanahitaji kuondoka kwenye nyumba hizi, lakini hawawezi kutimiza umri ambapo wanahitaji kutengana na familia.

Watoto wengi walioondoka kwenye makao ya watoto walitatizika kukubalika katika jamii. Kulikuwa na uwezekano mkubwa wao kujihuisha na shughuli za uhalfu, unyanyasaji wa kingono, matumizi ya madawa ya kulevyu na kufunga ndoa mapema maishani.

Nilijifunza kuwa chaguo la watoto kutunzwa na familia lilikuwa na faida kubwa kwa watoto. Tulianzisha shirika la kuasili watoto na mpango uliowasaidia watoto wakiwa na familia zao. Jambo hili lisisaidia kuimarisha familia na kuzuia kutengana. Mipango hii inaendelea kuwa na athari nzuri katika maisha ya watoto nchini Kenya.

**Ni nini kilichokusaidia kukabiliana na hata kupona madhara ya kukulia katika makao ya watoto?**

**WOKOVU NA NENO LA MUNGU –** Ninaendelea kufutilia kuwa na uhusiano wa kina zaidi na Mungu. Neno lake linajaa ahadi kubwa ambazo ninazitumia katika maisha yangu kila siku. Nimepata wokovu, uponyaji, furaha, nia na matumaini ndani yake.

**FAMILIA YANGU KANISANI –** Mimi ni mmoja wa wakikundi kinachoongoza katika sifa na kuabudu kanisani. Pia niko katika kikundi cha ushirika kinakutana kila wiki ambacho pia kina baadhi ya watu tuliokuwa

nao katika nyumba ya watoto yatima. Kikundi hiki cha ushirika kimekuwa familia yangu.

**MAKUNDI YA MSAADA –** Mimi nimejiunga na Shirika la Watu Waliokuwa katika Makao ya Watoto nchini Kenya, na bado ninawasiliana na ndugu na marafiki zangu amba tulikua pamoja. Jambo hili hunisaidia kukabiliana na madhara ya jinsi nilivolelewa.

Ni muhimu tuchague kusamehe na kusahau yaliyopita, na tuzingatie kazi ambayo Mungu anafanya ndani yetu na kuititia kwetu.

## MPANGO WA MUNGU WA KUTUNZA WATOTO NI FAMILIA

**Je, waweza kutueleza kuhusu kazi ya Child in Family Focus – Kenya?**

Mnamo mwaka wa 2011, nilihisi Mungu ananiita nijiunge naye katika kushughulikia maono mapya. Nilianzisha shirika la Child in Family Focus – Kenya ili kuhamasisha utunzaji uliojikita katika familia kwa watoto yatima na waliopitia hali ngumu nchini Kenya. Hili huwa tunafanya kuititia utetezi, kusaidia kuondo makao ya mayatima, na ufuutiliaji na usimamizi wa masuala ya huduma na ulinzi wa watoto.

Lengo letu ni kuteteta haki ya kila mtoto kupata nafasi ya kutunzwa akiwa katika familia. Maono yetu ni kuwa na nchi ambamo watoto yatima na waliopitia hali ngumu kupata utunzaji wakiwa katika familia, litakuwa ndilo jambo la kawaida na wala si nafasi wanayoipata wachache. Mnamo

mwaka wa 2016, shirika letu lilichangia pakubwa katika kubuniwa kwa Muungano unaotetea Utunzaji Mbadala (Alternative Care Alliance) – Kenya. Muungano huu unaleta pamoja watu binafsi, mashirika yasiyo ya kiserikali na serikali ili kushirkiana katika kutekeleza Mwongozo wa Utunzaji Mbadala wa Familia kwa Watoto nchini Kenya.

**Je, ni jumbe upi ambaou ungependa kuwapa wasomaji wa jarida la *Hatua kwa Hatua*?**

Ningependa kuwaambia kwamba 'Mungu huwakalisha wapweke nyumbani.' (Zaburi 68: 6). Mpango wa Mungu wa kutunza watoto ni familia. Ni mpango bora zaidi kuliko kuwatunza katika makao ya watoto – bila kujali nzuri wa nyumba ile au jinsi inavyoendeshwa vizuri.

Kwa wale wanaosaidia makao ya watoto, huu ni wakati wa kubadilisha mtazamo. Tia changamoto wale wanaosimamia makao ya mayatima wayabadilishe kuwa vituo vya kusaidia jamii. Vituo hivi vinaweza kuimarisha familia ili waweze kutunza watoto wao na jamaa zao walio yatima. Ikiwa utunzaji kutoka kwa jamaa na familia haupo au haufai, tunapaswa kuhimiza aina nyingine za utunzaji mbadala, kama vile familia za kulea na za kuasili.

Kwa kuhitimisha – Mungu haleti uchungu bila sababu, badala yake yeeye kufanya uchungu huo kuwa chanzo cha uzuri na nia.

---

*Peter Kamau Muthui ni mshirika mwanzilishi na mkurugenzi wa shirika la Child in Family Focus – Kenya.*

Tovuti: [www.childinfamilyfocus.or.ke](http://www.childinfamilyfocus.or.ke)  
Barua pepe: [peterk@childinfamilyfocus.or.ke](mailto:peterk@childinfamilyfocus.or.ke)

*Peter ni sehemu ya mpango wa Tearfund wa Watu Waliohamashwa, unaowasaidia viongozi wapya ambaou wanaleta mabadiliko katika jamii zao.*

Tovuti: [www.tearfund.org/inspired](http://www.tearfund.org/inspired)

Maelezo ya mawasiliano ya Shirika la Watu Waliokuwa katika Makao ya Watoto nchini Kenya:

Tovuti: [www.kesca.org](http://www.kesca.org)  
Barua pepe: [info@kesca.org](mailto:info@kesca.org)  
Simu: +254 721 612864



© Peter (anayeonyeshwa kwa mshale) na baadhi ya wengine katika nyumba ya watoto.



*Imeandikwa na Sarah Chhin*

# KUJITAYARISHA KUKABILIANA NA ULIMWENGU

*Shirika la M'lup Russey linabadiishi jinsi watoto walioptia mazingira magumu na vijana wanatunzwa nchini Cambodia. Tuna hamu ya kukuza njia mbadala kando na makao ya watoto na tunafanya kazi nyingi katika eneo hili. Lakini pia tunatambua kwamba inachukua muda kwa makao ya mayatima kubadilishi mkakati, na kwamba watoto wanahitaji msaada wakati bado wako katika makazi haya.*

## WOGA WA ULIMWENGU WA NJE

Katika mwaka wa 2007, wafanyakazi katika M'lup Russey waliandaa warsha na vijana zaidi ya 500 wanaoishi katika makao ya mayatima. Wote walizungumza kuhusu hofu walijokuwa nayo kuhusu kuondoka katika makazi hayo. Waliogopa kukabiliwa na unyanyapaa, kuonewa, kukosa kazi na makazi. Wengine waliogopa kuwa wangekufa njaa. Waliogopa kuwa hawakuwa tena na ujuzi wa kuwawezesha kuijunga na jumuiya huko nje.

La kusikitisha ni kwamba, kuna sababu za kutosha kuwa na hofu hii. Wasipoandalowi kwa makini, vijana wanaoondoka makao ya mayatima nchini Cambodia hutatizika kuijunga tena na maisha ya jamii na familia. Wamo katika hatari ya unyonyaji, unyanyasajji na biashara ya magendo. Makao ya mayatima hayaondoi hatari hii ya kunyanyaswa. Yanachofanya ni kuchelewesha athari zake.

Mara nyingi, hatari hii huongezeka kwa sababu yao kukaa katika makao ya mayatima.

Shirika la M'lup Russey huwasaidia watoto wakiwa bado wanaishi katika makao ya watoto – lakini kazi yetu haiishi pale. Sisi hufanya tuwezavyo ili kuwasaidia vijana kuijunga tena na jamii zao wanapoondoka kwenye makazi haya.

## KUJENGA MAHUSIANO

Kwanza, shirika la M'lup Russey hujenga mahusiano na wakurugenzi wa vituo vya makao ya watoto. Huwa tunawaalika katika mafunzo ili waweze kuboresha jinsi wanavyotunza watoto. Pia tunawasaidia kuelewa na kutekeleza sera ya serikali ya huduma mbadala, ambayo inasema kuwa njia ya kuwatunza watoto wakiwa katika familia ni bora zaidi. Katika miaka ambayo imepita, tumewafunza wakurugenzi wa makao ya mayatima kuhusu haki za watoto, ulini wa watoto, kushirikisha watoto, kudhibiti hasira, taratibu zinazofaa za kurejesha watoto katika jamii, usimamizi wa kituo, kuelewa mahitaji ya watoto na vijana, ujuzi wa uongozi na mengine.

Baada ya kujenga uhusiano na wakurugenzi, shirika la M'lup Russey linaweza kuanza kufanya kazi na watoto na vijana walio katika vituo vya wakurugenzi hawa. Huwa tunawapa

fursa ya kushiriki katika makundi ya kusaidiana wenyewe kwa wenyewe na mafunzo ya ujuzi wa maisha. Haya huwasaidia vijana kupata ujuzi wanaohitaji kuwa salama, kujitegemea na kushiriki katika jamii wanapoondoka katika vituo hivi.

## VILABU VYA VIJANA

Shirika la M'lup Russey huwasaidia vijana kuanzisha vilabu vya vijana katika vituo vyao. Shughuli za vilabu hivi husaidia vijana kujiamini zaidi na kuwa na uhuru na uwezo wa kuishi salama katika jamii katika siku zijazo. Wanachama wa klabu hujichagulia viongozi wao na kujiamulia muundo na ratiba zao. Vilabu hivi huwapa nafasi ya kujieleza katika vituo walimo. Vilabu hivi huwasaidia vijana kujieleza kwa uhuru na kuwaandaa kwa ajili ya maisha ya kujitegemea.

Yote haya huwafundisha jinsi ya kuwa viongozi, waratibu na wanakundi wanaowajibika. Huwasaidia kuboresha ujuzi wao wa mawasiliano na kazi, na kushirikiana vizuri na wengine. Kutokana na juhudhi za M'lup Russey, mamia ya vijana wamekuwa wanachama wa vilabu vya vijana yatima tangu mwaka wa 2008!

## MAFUNZO YA UJUZI WA MAISHA

Shirika la M'lup Russey pia huwafadhili vijana wanaoishi katika vituo hivi ili wapate mafunzo ya ujuzi wa maisha na wa kiufundi. Warsha hizi hufundishwa na wataalamu na wenyewe weledi. Wao hufunza mada za kina zaidi kama vile

- 'kujijua mwenyewe'
- ujuzi wa mawasiliano
- kuishi salama katika jamii
- kudhibiti hasira
- afya ya uzazi
- ufahamu kuhusu madawa
- matumizi bora ya pesa
- jinsi ya kupanga maisha
- kuijwekea malengo.

Mafunzo ya ujuzi wa maisha husaidia vijana kujifunza jinsi ya kuishi kwa kujitegemea wanapoondoka katika makao ya watoto. Picha: Shirika la M'lup Russey



## USAIDIZI ZAIDI

Huduma hizi za kusaidia zinapatia shirika la M'lup Russey fursa ya kujenga mahusiano mazuri na imara na watoto na vijana katika makao ya watoto. Kisha wanawenza kuwapa huduma zingine, kama ushauri nasaha na wa kisheria, pamoja na kuwasaidia wanapoondoka makao ya watoto.

## MTANDAO WA WALIOONDOKA MAKAO YA WATOTO

Shirika la M'lup Russey linaendesha Mtandao wa Walioondoka Makao ya Watoto kwa ajili ya vijana ambao wameondoka makazi haya ya watoto. Vijana hawa wanawenza kujinga na kikundi kidogo cha vijana wengine walio katika hali sawa. Katika mikutano wanayokutana mara kwa mara katika vikundi vidogo, wanawenza kushiriki hadithi zao na hali ya maisha yao katika jamii.

Pia kuna mikutano ya vikundi vikubwa, ambapo vikundi hivi vidogo huungana pamoja. Mikutano hii huwapa vijana hawa mtandao mkubwa wa watu ambao wanawenza kujenga mahusiano mazuri nao. Kupitia mtandao huu, vijana hawa husaidiana kujitegemea na kujichunga.

Vijana hawa wana nafasi ya pekee ya kuwasaidia wengine ambao hivi karibuni wataondoka makazi haya ya yatima. Wao hutembelea makao ya mayatima na kushiriki hali ya maisha yao katika jamii. Jambo hili huwasaidia vijana wengine yatima kutazama mustakabali wao wakiwa na matumaini zaidi. Shirika la M'lup Russey pia huwapa mafunzo ya kiufundi vijana walioondoka makao ya mayatima, hivyo kuwasaidia waweza kujitegemea maishani. Na mwishowe, kwa vijana ambao ni Wakristo,



• Vijana wakishiriki katika mafunzo ya ujuzi wa maisha juu ya kudhibiti hasira. Picha: Shirika la M'lup Russey

shirika M'lup Russey huwa na mafunzo ya Biblia na kundi la sala.



## MAWAZO YA JINSI YA KUTUMIA MAKALA HAYA

- Katika kikundi, jadili kile unachofikiri ni kizuri kuhusu njia inayotumiwa na M'lup Russey.

- Jadili njia ambazo kanisa, kikundi au shirika lako linawenza kusaidia watoto na vijana baada ya kuondoka katika makao ya watoto. Kwa mfano, kuna mitandao ya walioondoka makao ya watoto hapo awali kwenye eneo lako, ambayo unawenza kuwaelekeza vijana wajunge nayo?

Tovuti: [www.mluprussey.org.kh](http://www.mluprussey.org.kh)  
Barua pepe: [info@mluprussey.org.kh](mailto:info@mluprussey.org.kh)



## UCHUNGUZI KIFANI: HADITHI YA PITHOU

*Pithou alikulia katika makao ya mayatima huko Phnom Penh, Cambodia. Hapa anashiriki mawazo yake juu ya kupata ujuzi wa maisha ukiwa katika makao ya mayatima:*

'Kujifunza ujuzi wa maisha kulinionyesha njia mpya ya kuishi. Zamani, sikujali kuhusu mustakabali wangu kwa sababu nilikuwa na wali wa kutosha kula na mahali pa kuishi. Nilidhani sikuwa na uwezo wa kufanya vizuri katika masomo na hata mama yangu alisema nilikuwa mpumbavu!

Lakini sasa nimekuwa na fursa ya kuelezea hisia zangu na kupata marafiki mionganoni mwa watu wengine wanaoishi katika makao ya mayatima. Niliona wawili kati ya marafiki hao wapya wakisoma na kutia bidi. Nikaanza kujuliza maswali. Kisha nikaamua kutia bidii masomoni kwa ajili ya mustakabali wangu na wa nchi yangu. Sasa ninajua kwamba sisi sote tuna thamani kubwa kwa jumuiya, jamii na nchi yetu.

Watu hufikiria kwamba makao ya mayatima huwapa watoto kila kitu

wanachohitaji, lakini hawajui. Watoto katika makao ya mayatima hawana matumaini na hawana upendo wa wazazi wao. Mafunzo ya ujuzi wa maisha yamenifaa sana mimi. Yamefungua moyo na akili yangu. Yamenifunza kuwa na ujasiri na kushiriki mawazo yangu, jambo ambalo singewenza kufanya hapo awali kwani nilijihisi dhaifu na mwenye woga. Sasa najiona nina nafasi na uwezo.'

# KUIMARISHA FAMILIA

**Kuimarisha familia** kunahusu kuweka watoto katika familia zao na kuwazuia wasipelekwe katika makao ya watoto. Familia tofauti zitakuwa na mahitaji tofauti, na nyingi zitahitaji mchanganyiko wa mbini.

Makao ya watoto yatima yakibadilisha mkakati, yanaweza kutumia majengo na rasilimali zake kutoa huduma kwa jamii. Kanisa lako au kikundi cha jumuia kinaweza kushiriki na kuwa na jukumu muhimu katika kusaidia familia. Yafuatayo ni baadhi ya mapendekezo ...

## MSAADA WA KIELIMU

Mara nyingi familia maskini hutatizika kupata karo ya shule, vitabu na sare. Huenda wakafikiria kuwa mtoto atapata nafasi nzuri ya kupata elimu akiwa katika makao ya watoto. Kusaidia familia kugharamia mambo haya kunaweza kuleta tofauti kubwa. Jaribu kujadiliana na shule ili zipunguze au ziondolee karo watoto walio katika mazingira magumu. Tumia kituo chako cha jamii kuwapa watoto ambao hawana matokeo mazuri shulenii masomo ya ziada au fursa za kujifunza.



## SHUGHULI ZINAZOZALISHA MAPATO

Umaskini mara nyingi ndiyo sababu kuu inayofanya familia kuweka watoto katika makao ya mayatima. Kusaidia familia kutafuta njia za kuchuma kipato cha kutosha kunaweza kuleta tofauti kubwa. Waweza kutoa mafunzo ya kiufundi, kama kushona nguo, useremala, ufuaji vyuma, kuoka, kutengeneza nywele au uujuzi wa kompyuta. Mafunzo haya yanapaswa kuambatana na mahitaji na fursa zilizopo katika jamii. Wasaidie watu kuanzisha biashara ndogo ndogo na uanze kuwapa huduma za kuweka akiba na kupata mikopo.



## USHAURI NASAHA

Ushauri nasaha unaweza kusaidia familia na wazazi wanaopitia magumu kama vile kuvunjika kwa ndoa au matumizi ya madawa ya kulevya. Angalia kama kuna ye yote miiongoni mwa washiriki katika kanisa lako au jumuiya ambaye amehitimua na yuko tayari kutoa huduma hii. Kama sivyo, tafuta mshauri kutoka mahali pengine ambaye anaweza kuwa akitembea mara kwa mara ili kutoa ushauri.



## UWEZO WA KUPATA HUDUMA ZA AFYA

Kupitia kituo chako cha jamii, saidia familia zipate huduma za afya, ikiwa ni pamoa na kupima VVU na ushauri nasaha. Wape mafunzo watu waliojitelea ili waweze kutembelea wanafamilia wanaougua nyumbani na kuwatunza ili watoto waweze kwenda shule. Wape usaidizi walemvu, kwa mfano wasaidie kupata tibamaungo, aina nyingine za tiba kama ile ya lugha na kuzungumza.



## USAIDIZI KWA WAZAZI

Wape wazazi na walezi mafunzo katika mada kama vile ujuzi wa kulea watoto, kuandaa bajeti, lishe nzuri, ukuaji na ulinzi wa watoto. Kufanya hivi kutaimarisha familia na kuongeza imani yao katika kutunza watoto.



## VILABU VYA WANAWAKE, WANAUME NA WATOTO

Vilabu vya wanawake huwaruhusu kuja pamoja na kuzungumza kuhusu hali na changamoto zao. Vilabu vya watoto huwapa nafasi ya kusaidiana na kujieleza. Anzisha na uwezeshe vilabu hivi – na ufikirie kuhusu kuanzisha kikundi cha wanaume pia, kitakacholenga kujadili suala la kinachomfanya mtu kuwa baba mzuri.



## VITUU VYA KUWACHUNGA WATOTO VYA BURE AU KWA GHARAMA NAFUU

Jitolee kuwachunga watoto wakati wa mchana. Kufanya hivi kutawawezesha wazazi au walezi kwenda kazi na kuweza kusaidia familia zao. Wapatie watoto chakula, shughuli zinazowachangamsha na muda wa kucheza mchana. Jitolee kuwachunga watoto wenye ulemavu ili kuwapa wazazi wao nafasi ya kupumzika.



## MIPANGO YA KUFIKIA JAMII

Wafunze watu waliojitelea kutembelea familia zinazoathirika nyumbani mwao na kuwapa msaada wanaohitaji. Wanaweza kusaidia kwa mambo kama vile maandalizi ya chakula na kazi za nyumbani, pamoja na msaada wa kihisia na kiroho.



## UTETEZE NA UPATAJI HUDUMA

Wasaidie yatima na walezi wao wapate faida wanazostahili, kama vile misaada na huduma za serikali. Wakati mwingine wanahitaji tu kujulishwa misaada na huduma zinazopatikana. Huenda watoto yatima wakahitaji pia kusaidiya kupata haki za urithi, nafasi katika shule au hati za utambulisho. Chagua wawakilishi kutoka kundi lako la jumuia watakaotetea mahitaji ya watoto waliopitia mazingira magumu, katika mikutano ya bodi za shule na halmashauri za mitaa.

# MAKAO YA MAYATIMA YALIYOBADILIKI KABISA

*Ujumbe unaenea kwamba kuishi katika makao ya watoto kwa muda mrefu hakuwafai sana yatima na watoto waliopitia mazingira magumu. Kutokana na hayo, makazi mengi ya yatima duniani yanabadiishiwa na kufanywa vituo vya kutoa huduma za kuimarisha familia na jamii. Utaratibu huu mara nyangi unaitwa 'kubadilishi mkakati'. Rebecca Nhep, Mkurugenzi wa ACC International Relief, anaeleza jinsi mabadiliko haya yanaweza kufanya.*

## KUBADILISHA JINSI TUNAVYOTUNZA

Ikiwa umekuwa ukisaidia au una makao ya mayatima au nyumba ya watoto, wazo la kubadilisha mkakati huo na kuanzisha mfumo unaoshughulikia familia na jamii linaweza kuwa la kutisha sana. Suala hili linaibua maswali mengi kama vile, 'Kubadilishi mkakati kunahusisha nini?', 'Ninawezaje kuhakikisha kuwa watoto wako salama na wanatunzwa vizuri katika familia?', 'Je, na kuhusu elimu au imani yao?', 'Je, wafadhili wangu watafikiri nini?', 'Tutafanya nini jengo letu ikiwa watoto hawaishi hapa tena?' na 'Nitafanya nini na huduma yangu tukiacha kuwa na makao ya mayatima?'

Wakati mwagine maswali na wasiwasi huu huhisi kama viwkazo vinavyotuzua kubadilisha. Hata hivyo, ukipanga vizuri, upate msaada unaohitaji na taratibu zilizoandaliba vizuri, unaweza kuhakikisha mabadiliko haya yametimia na ni salama kwa watoto. Zaidi ya hayo, utaona ongezeko katika mafanikio na idadi ya wale wanaofikiwa na mpango au huduma yako.

Mpango wa Kinnectd wa ACC International Relief unasaidia mashirika ya ndani mwa nchi na ya kimataifa katika kubadilisha mkakati wa makao yao ya watoto. Katika kipindi cha miaka sita iliopita, tumefanya kazi na zaidi ya makazi 60 ya watoto katika nchi 11 tofauti.

Hadithi ya Mchungaji Myint Nwe inaonyesha baadhi ya hatua muhimu zinazohusika katika kubadilisha. Huu ni mfano mmoja tu wa jinsi mchakato huu unavyoweza kufanyika.

## KUFAHAMU HAJA YA KUBADILISHA

Mchungaji Myint Nwe ni mkurugenzi wa Caring and Loving Children (CLC), shirika la kijamii nchini Myanmar. Alikuwa anasimamia vituo tano vya makazi kwa watoto vilivyo katika maeneo mbalimbali nchini. Wengi wa watoto katika vituo hivi walikuwa na jamaa hai, lakini walikuwa wamepelekwa pale kwa sababu ya umaskini uliokithiri, kifo cha mzazi mmoja au wote wawili, au hali nyiningine ya mgogoro.

Baada ya muda, Mchungaji Myint aliona kuwa kuishi katika makazi haya halikuwa jambo nzuri kwa watoto hawa. Aligundua kuwa, wakati wowote ikiwezekana, watoto walifaa kuishi na familia zao. Hata hivyo, hakuwa na ujuzi na utaalamu uliohitajika kubadilishi vituo hivyo na kuwarudisha watoto katika jamii. Shirika la Kinnectd lilikubali kusaidia na kuongoza CLC katika mabadiliko ya kuwa kituo kinachohimiza utunzaji watoto wakiwa katika familia.

► **MAELEZO YA KUMBUKA: Ni muhimu mtu awe na uhakika kuwa kuna haja ya kubadili**

## KUWAANDAA WASHIRIKI MUHIMU

Kwanza, shirika la Kinnectd lilisaidia CLC kufikiri juu ya kuandaa washiriki wakuu kabla ya kufanya mabadiliko yoyote muhimu. Washirika hawa ni pamoa na wafadhili, wanachama wa bodi, wafanyakazi, viongozi wa jumuiya na wale wa serikali za mitaa.

► **Watoto katika mpango wa miaka ya mapema huko Myanmar. Majumba ya watoto yanaweza kubadilishi mkakati na kuanza kutoa huduma za jamii kama hii. Picha: Alice Keen / Tearfund**



► **MAELEZO YA KUKUMBUKA: Ni muhimu kuelimisha kila mtu anayehusika kuhusu haja ya kubadilisha na kuanzisha utunzaji ndani ya familia, na jinsi mabadiliko haya yanaweza kufanyika. Kusisitiza faida kwa watoto kunaweza kusaidia katika kushawishi watu.**

## KUJENGA UWEZO

Hatua nyiningine ambayo Kinnectd ilichukua ilikuwa kujenga na kuimarisha uwezo wa Mchungaji Myint kama kiongozi wa CLC. Kuanzia mwaka wa 2013, alienda nyanjani kukutana na mshirika mwagine wa Kinnectd ambaye alikuwa anafanya kazi ya kuimarisha familia mazingira sawa. Jambo hili lilimsaidia ajionee manufaa ya kuunganisha familia, kupangia watoto kupata familia za kulea au kutunzwa na jamaa zao, na kijiunga na mitando ya wenzake.

► **MAELEZO YA KUMBUKA: Ni muhimu kwa viongozi wa makao ya mayatima kutafakari jinsi mabadiliko haya yatakavyoonedana katika jumuiya yao. Huenda viongozi hawa wakahitaji mafunzo ya ziada katika mada kama vile ulini wa watoto, ukuaji wa watoto, usimamizi wa kesi, kutunza mtoto akiwa katika familia na namna ya kufuatilia na kutathmini. Wanapaswa kutafuta njia za kuungana na idara za serikali na mashirika mengine yanayoshughulikia ustawi wa watoto, ili waweze kufanya kazi vizuri pamoja.**

## KUPANGA KWA AJILI YA MABADILIKO HAYA

Kwa pamoja, mashirika ya Kinnect na CLC yaliandaa mpango wa kubadilisha mkakati wa shirika hili. Shughuli hii ilihusisha kuandika lengo, maono, nguvu, malengo ya baadaye na mwelekeo, matokeo ya kupima, shughuli, rasilimali, na maeneo ambapo CLC ilihitaji elimu au uzoefu. Shirika la Kinnect liliwapa mafunzo wafanyakazi wa CLC ili kuhakikisha wangeweza kusaidia mchakato huo na walikuwa na ufahamu na ujuzi uliohitajika.

► **MAELEZO YA KUKUMBUKA:** Ni muhimu kuanda mpango wa kina kuhusu jinsi mabadiliko ya shirika yatakayofanyika. Ni muhimu kuajiri wafanyakazi wa kijamii na kuhakikisha kuwa wana ujuzi unaohitajika. Huenda wataalam wakahitaji mafunzo ya njia za kufanya kazi na watoto waliopitia mazingira magumu na walezi wao. Baadhi ya mada ni kama kuchunguza, kutathmini, kutafuta familia (njia za kupata jamaa za watoto) na kubuni ramani ya huduma zinazopatikana.

## HATUA KATIKA KUBADILISHA MKAKATI

Wakati wowote alipoweza, Mchungaji Myint alitafuta wanafamilia wa mtoto aliyekuwa anachunga. Kisha yeye na timu yake walipima iwapo walifaa na walikuwa tayari kumchunga mtoto huyo inavyostahili.

Mchungaji Myint alijua kwamba umasikini ndiyo sababu ilifanya baadhi ya watoto wapelekwa katika makao ya watoto. Kwa hivyo aliwasaidia wanafamilia kuanzisha biashara ndogo kama vile kushona nguo, maduka ya mboga na kilimo cha mifugo. Pia familia ziliunganishwa na mifumo ya kutoa usaidizi au huduma nyingine za jamii.

Mchungaji Myint alianza na nyumba tatu za watoto yatima ambapo kanisa lililokuwa linafadhili lilikuwa tayari kubadilisha mkakati. Kulikuwa na jumla ya watoto 53 katika nyumba hizi. Kufikia sasa, amewarudisha watoto wawili katika familia zao halisi na kuwaweza 22 chini ya utunzaji wa jamaa zao. Vijana wawili wakubwa wamehama na kuanza maisha ya kujitegemea huko wakipokea msaada kiasi.

► **MAELEZO YA KUKUMBUKA:** Ni muhimu kuweka watoto salama katika mchakato huu. Familia zinapaswa kuchunguzwa vizuri kabla mtoto hajapelekwa pale. Chaguo bora zaidi ni kuwaunganisha watoto na familia zao halisi, lakini kama chaguo hili si salama au halifai, chaguo zingine zinatafaa

## 'NINGEPENDA KUBADILISHA NYUMBA YANGU YA WATOTO YATIMA! NINAHITAJI KUFANYA NINI?

Majumba mengi ya yatima yatahitaji msaada wa kiufundi kutoka kwa shirika kama vile Kinnect ili kuwasaidia kutekeleza mabadiliko vizuri. Msaada huu unayawezesha kuweka mifumo sahihi ili kuweza kubadilisha bila matatizo.

Majumba ya yatima ambayo yako tayari kubadilisha mkakati yanaweza kuwasiliana na Kinnect (tazama maelezo ya mawasiliano hapa chini). Kisha shirika la Kinnect litatathmini kiwango cha msaada linachowezwa kutoa.

Rasilimali inayoweza kusaidia ni mwongozo wa utaratibu wa watoto kujiunga na familia ulioandaliwa na shirika la Faith to Action. Tembelea [www.faithtoaction.org/resources](http://www.faithtoaction.org/resources) ili upakue nakala ya bure.

kuzingatiwa. Chaguo hizi zaweza kuwa kutunzwa na jamaa wengine, kutafuta familia za kulea au za kuasili.

Mpango wa utunzaji wa kila mtoto huandaliwa na huonyesha yale yanayofaa kufanya ili kutayarisha mtoto kujiunga na familia. Baada ya hapo, mpango wa kusaidia familia huandaliwa. Mpango huu hubainishwa mabadiliko na msaada unaohitajika ili kuruhusu mtoto na familia kutekeleza mabadiliko yanayohitajika kwa mafanikio.

Mchungaji Myint na mfanyakazi wa kijamii kutoka CLC mara kwa mara hufuatilia watoto wote ambao wamewekwa katika familia. Utaratibu wa kufuatilia hupungua kadri muda unavyopita katika kesi za watoto ambazo zinaendelea sambamba, hadi wakati zinapofungwa. Utaratibu huu huchukua angalau miezi 12, na wakati mwingine muda zaidi. Wanaofatilia hupanga ziara za kufika kwenye familia husika lakini wakati mwingine wao hupiga simu kati ya ziara moja na nyingine (hasa kwa watoto walio katika maeneo ya mbali). Iwapo wakati wa ziara wafanyakazi wa kijamii watatambua haja ya kutoa msaada wa ziada, wao hupanga ili msaada huo ufikie familia inayouhitaji.

► **MAELEZO YA KUKUMBUKA:** Baada ya watoto kuunganishwa tena na familia zao, kuna haja ya kufuatilia ili kuhakikisha mambo yote yako sambamba na mtoto ako salama.

Shirika la CLC sasa limefunga kabisa makao yao ya kwanza ya watoto yatima. Makazi hayo yamebadilisha na kuwa kliniki ya afya ya familia na kituo cha kujifunza cha jamii. Kituo hiki hutoa mafunzo ya kiufundi, ambayo husaidia wanajamii kupata ajira au kuanzisha biashara zao ndogo. Jambo hili linaweza kusaidia kuzuia kuvunjika kwa familia.

Mchungaji Myint pia ameanzisha huduma ya dharura ya kulea watoto ili kutoa utunzaji wa muda kwa watoto walioandaliwa au wanaoteswa. Watoto hawa huletwala pale na polisi au viongozi wa jamii. Mchungaji Myint na mfanyakazi wa kijamii anayeshirikiana naye huanza mchakato wa kutafuta na tathmini familia. Lengo lao huwa kupata familia inayofaa, salama kwa ajili ya mtoto, iwe kwa njia ya kumuunganisha na familia yake, jamaa zake au kupata familia ya kumlea.

► **MAELEZO YA KUKUMBUKA:** makao ya watoto yanapobadilisha mkakati, majengo na rasilimali zilizopo zinaweza kutumiwa kutoa huduma za kuimarisha familia na jamii.

## UBIA

Sasa Mchungaji Myint ni mtetezi wa kuwatunza watoto wakiwa katika familia, na husimulia aliyojifunza kwa wakurugenzi wengine wa makao ya mayatima. Yeye ni sehemu ya kikundi kinachofanya kazi kutoa njia mbadala nchini Myanmar.

Rebecca Nhep ni mmoja wa Wakurugenzi Watendaji Wakuu na Mkurugenzi wa Mipango ya Kimataifa katika shirika la ACCI Relief.

Tovuti: [www.kinnect.org.au](http://www.kinnect.org.au)  
Barua pepe: [info@kinnect.org.au](mailto:info@kinnect.org.au)  
Anwani: 5/2 Road Sarton, Clayton,  
Victoria 3168, Australia  
Simu: +61 3 8516 9600

Makala haya yalitolewa kwenye mifano ya CAFO ya kuwaunganisha watoto na familia za kuwatunza. Angalia [www.cafo.org/resource/replicable-models-for-transition-to-family-based-care](http://www.cafo.org/resource/replicable-models-for-transition-to-family-based-care)

# KUTUMIA SANAA KAMA TIBA

## KWA YATIMA NA WATOTO WALIO KATIKA MAZINGIRA MAGUMU

Kubuni sanaa na kuizungumzia kunaweza kusaidia watoto kupona athari zozote zinazotokana na hali ngumu waliyoipitia. Shughuli hizi zinaweza kujumuisha kuchora picha za kawaida na za rangi, ufinyanzi, kolaji na aina yoyote ya sanaa. Shughuli zifuatazo zinaweza kusaidia yatima na watoto walio katika mazingira magumu kuelezea hisia zao, kujithamini zaidi na kukabiliana na kumbukumbu ngumu.

Anayemtunza mtoto kama yule anahitaji kusikiliza vizuri, kumwonyesha kuwa anamwelewa, anamkulabi kikamilifu na anampenda. Ni muhimu kuwa makini kwa kiasi ambacho mtoto ako tayari kushiriki ama kuzungumzia. Mazingira yanafaa kuwa huru na ya kirafiki, na watoto wanapaswa kuwa na furaha wakati wanashiriki katika shughuli hizi (kwa mfano kutumia rangi na vifaa tofauti).



### NJIA YA 1: MAHALI SALAMA

*Njia nzuri ya kuanza na watoto ambao wamepatwa na shida fulani iliyowatia kiwewe ni kuwafanya wachore 'mahali salama'. Shughuli hii pia inafaa kwa watoto ambao wanapatwa na wasiwasi.*

Mhimize mtoto afunge macho na afikirie kuhusu mahali ambapo anajihisi salama sana. Panaweza kuwa mahali halisi au pa kubuni. Mpe muda mwingu wa kufikiria mahali hapo; hatua hii inaweza kuwa ngumu kwa watoto waliopitia hali ngumu hivi karibuni. Mwambie kuwa watu walio pale ni wale pekee ambaao angetaka, na hakuna

chochote kibaya kinachoweza kumfikia. Muulize maswali ya kumsaidia kubuni picha ya mahali hapo, kama vile, 'Angalia mahali pale. Unaona nini? Pananukia aje? Unasikia nini? Una furaha nyingi na uko salama ... Unafanya nini? 'Uliza 'Kuna nini kingine?' ili kumhimiza mtoto kutoa maelezo zaidi. Mtoto akimaliza kutafakari mahali hapo, anaweza kupachora au kupatengeneza kwa kalamu za rangi, penseli, rangi au vifaa tofauti. Mhimize akumbuke mahali hapo na apafikirie wakati wowote anapohisi woga au huzuni.

### NJIA YA 2: HUYO NI MIMI!

*Shughuli hii inaweza kuimarisha jinsi mtoto anavyoitambua na kumsaidia kujiamini zaidi.*

Mfanye mtoto aangalie kioo. Wakati anaangalia, muulize maswali yafuatayo:

- Unaona nini?
- Ni nani aliyekuumba?
- Ni watu wangapi ulimwenguni wanaofanana na wewe? (Mweleze mtoto kwamba Mungu alimuumba mtoto kwa njia ya pekee. Mwambie kuwa chochote kilichotoka mikononi mwa Mungu ni kizuri na kirembo – ikiwa ni pamoja na mtoto huyu.)
- Unakaa vipi? Je, unaweza kujieleza?
- Unapenda nini kujihu? Una nini cha kipekee?

Kisha tengeneza aina yoyote ya sanaa yenye mtoto huyu kulingana na aliyokwambia. Yafuatayo ni mapendekezo kadhaa, lakini unaweza kubuni yako mwenywewe.

- Mwelekeze mtoto aguse rangi au wino usio na sumu kwa kiganja cha mkono wake, kisha mfanye aweke mkono huo katikati ya kipande cha karatasi. Vinginevyo, mtoto anaweza kuchora mkono wake kisha apake picha ile rangi.
- Mwelekeze mtoto aandike juu au karibu na mchoro ule wa mkono, 'Mimi ni wa pekee.'
- Kuhimiza mtoto aandike juu ya kila kidole cha mkono mambo anayopenda kujihu.
- Mpime mtoto kisha aundike matokeo pamoja na tarehe kwenye karatasi.
- Mwelekeze mtoto aweke kipande cha nywele zake kwenye karatasi kwa gundi.

Hii inaweza kuwa sehemu ya shughuli za sanaa juu ya mada kama vile 'Mahali nilipo sasa', 'Urafiki' na 'Matumaini yangu ya baadaye'. Watoto wanaweza kukusanya sanaa hizi kwenye folda na kupamba jalada la folda.



Mfano: Amy Levene/Wingfinger

Julie Hefti alisomea jinsi ya kutibu kuitopia burudani na amefanya kazi na watoto wanaoishi na familia za kulea. Pia amefanya kazi nchini Kenya na wasichana wa Kimaasai walipatwa na kiwewe, nchini Uswisi na watumiaji wa madawa ya kulevyia na huko Jordan katika shule za chekechea za watoto wakimbizi kutoka Syria. Barua pepe: ps9213@googlemail.com

KABLA YA  
KUANZA  
Tafuta nambari ya mshauri  
aliyehitimu kutoka eneo  
hilo ambaye anafanya kazi na  
watoto. Watoto wakionyesha  
dalili za dhiki, simamisha  
shughuli, wafariji na uone kama  
unaweza kupanga wakutane  
na mshauri huyo.

## NJIA YA 3: KUBADILI KUMBUKUMBU

*Shughuli hii inaweza kusaidia watoto kubabiliana na mambo ya kutisha yaliyotokea katika maisha yao.*

Kuruhusu watoto kuchora kwa kalamu au kwa rangi chochote wanachochagua na kumakinikia kile wanachobuni, kutawasaidia kuelezea mawazo na hisia zao. Uliza maswali kama vile, 'Nieleze kuhusu picha yako', 'Ni nani uliyechora pale?' na 'Anafanya nini?' Ikiwa shughuli hii itaonyesha kuwa mtoto huyo anaogopa, unaweza kutumia shughuli ifuatayo.

Msimulie mtoto hadithi kuhusu watu au wanyama waliogopa sana kitu fulani. Katikati ya hali hii, kitu fulani kilitokea

kilichowatoa hatarini. Pengine mtu au mnyama mwinge aliukua na hofu yao ikatoweka. (Mfano kutoka Biblia ni hadithi ya Yesu kutuliza dhoruba wakati wanafunzi walikuwa na woga.)

Rudi kwenye picha ambayo mtoto alichora ya wakati aliukua na woga. Muulize ni nini kilichomsaidia katika hali hii na kilichomfanya aache kuwa na woga. Ikiwa mtoto ameshindwa kutambua chochote kilichomsaidia, mhimize kufikiri kitu fulani kwa kuuliza, 'Ni nini kilichokusaidia?' Mwambie mtoto achore mtu huyu au kitu hiki ambacho kilimsaidia kwenye picha, ili kubadilisha kumbukumbu.



*Imeandikwa na Godfrey Turyatemba na Susan M. Otai*

## KUUNGANISHA WATOTO NA FAMILIA ZAO

*Kuunganishwa tena kuna maana ya kuwasaidia watoto kurudi katika familia na jamii.*

Watoto na familia wanahitaji kusaidiwa kwa makini kabla ya kuunganishwa tena. Mchakato utakaofuata utategemea hali yao ya kipekee. Ni muhimu mchakato huu usiharakishwe. Kwa watoto ambao wamekuwa mitaani au katika taasisi kwa muda fulani, mchakato huu mara nyiningi huchukua angalau miezi sita.

Mtoto hufuata mchakato huu:

- **Uokoaji:** Watoto wanaweza kuletwa kutoka hospitali, kuelekezwa na wafanyakazi wa kijamii au polisi. Wakati mwinge watoto wachanga hupatikana kwenye mapipa ya taka au kando ya barabara.

- **Kuwezesha kuishi maisha ya kawaida:** Wafanyakazi wa kijamii wanapaswa kumfanya mtoto tathmini ya mwanzo. Tathmini hii huonyesha hali ya mtoto kimwili, kiakili, kihisia, kiafya na kisaikolojia. Mahitaji ya haraka hutambuliwa na kushughulikiwa kabla ya kumrejesha mtoto ndani ya familia.

- **Mpango wa Utunzaji:** Mpango wa utunzaji unapaswa kuwa na taarifa kuhusu mahitaji ya mtoto na jinsi atakavyounganishwa na familia au jamii. Pia una maelezo ya muda, mtu atakayehusika, ghamama na hatua za kukamilisha uhamishaji wa mtoto. Ni muhimu kuwasaidia watoto kuijandaa kihisia kuunganishwa tena na familia au jamii.

Kazi inayohusu familia inajumuisha:

- **Kuitafuta familia:** Wafanyakazi wanaohusika huitafuta familia halisi ya mtoto au kutafuta familia ya kulea. Wao hutembelea familia hii na kuzungumza juu ya mtoto.

- **Tathmini na maandalizi:** Wafanyakazi wa kijamii hutathmini kama familia inaweza kumtunza mtoto bila kumtia hatarini.

- **Kutembelea familia:** Mtoto huyu hutembelea familia na kuanza kujuana kabla hajaenda kuishi nao kabisa.

- **Kujenga mitandao ya usaidizi:** Ziara hupangwa ili kuunganisha familia na huduma za usaidizi zilizo karibu. Huduma hizi zinatoka kwa wafanyakazi wa afya, wale wa kijamii na viongozi wa jamii na wa kidini.

Hatua hizi zikishachukuliwa, mtoto anaweza kuijunga na familia. Baada ya mtoto kuijunga na familia, mfanyakazi wa kijamii anafaa kutembelea familia hiyo ndani ya siku saba ili aone jinsi wanavyoendelea. Mfanyakazi wa kijamii atatembelea familia mara kwa mara hadi mtoto huyo atakapokuwa amejiunga na familia kikamilifu. Kwa kawaida ziara hizi hufanyakazi mara moja kwa mwezi kwa miezi mitatu ya kwanza, na mara moja kila baada ya miezi mitatu kwa hadi mwaka moja, kulingana na hali ya familia. Shirika husika linapaswa kuwasiliana na mtoto hata baada ya mtoto kuondoka katika mpango huo.

*CRANE ni mtandao wa mashirika ya Kikristo nchini Uganda na mhirika wa Viva. Wao hulenga kuhamasisha mabadiliko ya kudumu katika maisha ya watoto kupitia hatua za pamoja.*

*Tovuti:* [www.cranenetwork.org](http://www.cranenetwork.org)  
*Barua pepe:*  
[administrator@cranenetwork.org](mailto:administrator@cranenetwork.org)

# WAKATI 'KULEA' NI NENO JIPYA

Casa Viva ndio shirika pekee linalojitahidi kutekeleza upataji familia za kulea nchini Costa Rica. Kwa ushirikiano na makanisa yaliyo karibu, wao huhimiza familia kujitolea kukaribisha watoto wenyewe mahitaji nyumbani mwao.

Philip na Jill Aspegren walianzisha Casa Viva katika mwaka wa 2003. Kabla ya hapo, wao walikuwa na mji wa watoto katika Jamhuri ya Dominika kwa miaka sita. Ingawa walipenda kazi yao, walijuliza kama kulikuwa na njia mbadala bora kuliko huduma za makazi. Katika mwaka wa 2003, shirika la Viva liliwaalika Philip na Jill Aspegren kutafiti swali hili katika Amerika ya Kati.

Philip na Jill walichagua kufanya utafiti huu Costa Rica. Walipoanza, 'kulea' lilikuwa neno geni nchini Costa Rica.

## HATUA ZA KWANZA

Philip na Jill walianza kwa kujenga mahusiano na serikali ya mitaa na ya kitaifa. Walipitia sheria na sera za Costa Rica ili kuona walichokubaliwa kufanya. Kisha wakaanza kusimulia maono yao makanisani. Shirika la Casa Viva lilajiri wafanyakazi waliohitimu, kama vile wafanyakazi wa kijamii na kubuni mtaala wa mafunzo kwa ajili ya makanisa na familia.

Baada ya miezi nane, mtoto wa kwanza alijunga na familia moja kutoka kanisa la

karibu. Tangu wakati huo, zaidi ya watoto 400 wamepata familia za kulea kupitia jitihada za Casa Viva. Sasa, idara ya ulinzi wa watoto mara kwa mara huwatumua watoto katika shirika hili.

## MIKAKATI

Shirika la Casa Viva daima huanza kwa kuweka mtoto katika familia ya kulea kwa muda mfupi. Hatua hii husaidia kukidhi mahitaji ya mtoto kwa wakati huo, huku likitafuta suluhisho la kudumu. Chaguo la kwanzla la Casa Viva ni kuunganisha watoto na familia zao halisi na kuwapa usaidizi unaofaa. Lakini katika hali ambapo hili haliwezekani au si salama, wao hutafuta suluhisho la kudumu kupitia kutafuta familia ya kumuasili mtoto. Ikiwa hakuna familia yoyote itakayopatikana na kumuasili mtoto, wao hutafuta familia za kulea za muda au za kudumu.

Kushirikiana na makanisa yaliyo karibu ni sehemu msingi ya kazi ya Casa Viva. Wao wamegundua kuwa makanisa yanaongozwa na wazo la Kibiblia la kuwakaribisha wale wenyewe mahitaji. Makanisa huwa na wajibu wa kutafuta familia za kulea, na wao husaidia familia hizi watoto wakishapelekwa mle. Wafanyakazi wenyewe ujuzi kutoka Casa Viva hufanya tathmini ili kuhakikisha kuwa watoto wamepatana na familia zinazofaa, na kusaidia kuandaa na kuongoza familia husika.

Washiriki kutoka Honduras, Panama, Costa Rica na Jamhuri ya Dominika wakimalizia kozi ya mafunzo ya Casa Viva. Picha: Casa Viva



## KUENEZA UJUMBE

Kubadilisha mtazamo linaweza kuwa jambo ngumu sana. Sasa Casa Viva hutoa mafunzo kwa makanisa, mashirika na serikali kutoka nchi nyingine za Amerika ya Kusini. Philip na Jill hukubali kujibu maswali kuhusu kozi zao za mafunzo, ambazo zinapatikana katika Kiingereza na Kihispania.



## MAPENDEKEZO YA KUTUMIA MAKALA HAYA

- Katika kikundi, jadili iwapo kuna familia nyingi zinazolea mahali unapoishi. Je, watu katika kanisa lako au jamii wanaweza kukubali kuwa familia za kulea kwa watoto yatima na wale walio katika mazingira magumu? Ikiwa wanaweza, unafaa kuwasiliana na nani ili kuanza mchakato huo?

*Shukrani kwa Philip na Jill Aspegren. Makala haya yaliandaliwa kwa kutumia mifano ya CAFO ya kuwaunganisha watoto na familia za kuwatunza. Angalia [www.cafo.org/resource/replicable-models-for-transition-to-family-based-care](http://www.cafo.org/resource/replicable-models-for-transition-to-family-based-care)*

Tovuti: [www.casaviva.org](http://www.casaviva.org)  
Barua pepe: [cafecito@casaviva.org](mailto:cafecito@casaviva.org)



## UCHUNGUZI KIFANI: 'FAMILIA, KWA AJILI YANGU?'

*Wakati mama na bibi wa Rosa\* walifariki, hakuwa na ye yote wa kumtunza. Alipelekwa katika makao ya mayatima, ambapo ilionekana angekaa katika kipindi kilichosalia cha utoto wake.*

Mwaka mmoja baadaye, Stefano na Marielos waliskia kisa cha Rosa. Walikuwa wamepokea mafunzo ya Casa Viva na walikuwa tayari kumkaribisha nyumbani mwao kwa muda mrefu.

Mfanyakazi wa kijamii wa serikali alimwambia Rosa habari hizi. Kwanza, Rosa alishangaa sana hata hakuweza kuzungumza. Hatimaye akasema, 'Familia, kwa ajili yangu? Kwa ajili yangu mimi, wakati tayari ni mzee kiasi hiki? ' Watoto wenyewe umri wa miaka kumi na moja katika hali yake wana nafasi ndogo sana ya kuishi na familia.

Siku ya kwanza ya Rosa na familia yake mpya, alipata sanduku la vifaa vyaa sanaa. Alicheza

na 'dada' yake mpya na kueleza hisia zake kupitia sanaa yake.

Usiku huo, Stefano na Marielos walipoenda kulala, walipata kazi ya sanaa ya Rosa (hapo juu) ikiwa imefichwa chini ya shuka. Alikuwa amechora picha ya familia, na amejiweka katika familia mpya. Sasa aliwa na familia.

\*Majina yamebadilishwa.





Watoto wengine wana familia kubwa. Baadhi wana familia ndogo. Wengine ni yatima. Hii inamaanisha kuwa mama au baba zao wamefariki au hawawachungi tena. Watoto wengine wanasubiri familia ili wapate mahali pa kuishi.

Lakini Biblia inasema kwamba Mungu anataka kutuchukua sisi sote kama watoto wake maalum! Hii inamaanisha kuwa kamwe hatufai kujihisi wapweke. Daima tunaweza kuzungumza na Mungu kuhusu chochote tunachofikiria na kuishi.

Tafuta maneno haya yaliyofichwa kwenye mchoro huu

Maneno yanaweza kwenda juu, chini, mbele, nyuma au kutoka pembe moja hadi nyingine.

Hatutaki watoto yatima wajihisi ...

WENYE UPWEKE      WENYE HUZUNI

WENYE WOGA      TOFAUTI

Tungependa watoto yatima wajihisi ...

WAMEPENDWA      WENYE FURAHA

SALAMA      KAWAIDA

## SISI SOTE NI SEHEMU YA FAMILIA YA MUNGU

Je, unajua watoto wowote ambao huenda wanajihisi wenye upweke? Unawezaje kuwasaidia kujihisi vyema zaidi? Andika mawazo yako hapa chini.

H	A	B	A	K	I	L	W	E	N	D	W
A	W	E	N	Y	E	U	P	W	E	K	E
T	E	F	M	C	H	H	W	S	A	A	N
U	N	H	T	O	V	U	T	A	S	M	Y
T	Y	A	K	A	M	F	U	L	Z	W	E
W	E	N	Y	E	W	O	G	A	W	A	F
T	H	O	T	W	E	N	M	Y	E	U	
J	U	K	A	W	A	I	D	A	Y	M	R
K	Z	A	T	O	F	A	U	T	I	E	A
S	U	I	K	U	Y	A	W	E	K	P	H
Z	N	U	N	W	A	L	E	W	E	N	A
A	I	W	A	M	E	P	E	N	D	W	A



### ZOEZI LA KUWEKA MSTARI KUTOKA BIBLIA KWENYE KUMBUKUMBU!

Je, unawezaza kujifunza kukariri mstari huu wa Biblia?

Nitakuwa Baba kwenu, nanyi mtakuwa kwangu wanangu wa kiume na wa kike, asema Bwana Mwenyezi. (2 Wakorintho 6:18)



Imeandikwa na Jude Collins

# KUTETEA HAKI ZA YATIMA

## MASOMO KUTOKA ASIA YA KATI

*Kuanguka kwa Umoja wa Kisovyeti katika mwaka 1991 kulifanya familia nydingi katika nchi za Asia ya Kati zivunjike. Jambo hili lilifanya idadi kubwa ya watoto wapelekwe katika makao ya mayatima.*

Rafiki kutoka Asia ya Kati anaeleza: 'Katika kipindi cha wiki moja, watu walipoteza kila kitu. Viwanda vilifungwa na hakukuwa na pesa za kulipa mishahara. Wanaume wengi waliteseka sana. Wakaanza kunywa pombe na madawa ya kulevy. Wanawake wakajipata wakihitajika kuchukua jukumu la kutafutia familia zao riziki na wengi wakaenda Ursusi kutafuta kazi, jambo ambalo hawakulitarajia. Watoto waliachwa kwa jamaa, majirani au hata wageni. Wengi wao wakaishia bila makazi au katika makao ya mayatima. Sasa, maelfu ya watoto wako katika makao ya mayatima au wanaishi mitaani.'

Watoto wanapofikia umri wa miaka 16, wanatarajiwa kuondoka kwenye makao ya mayatima. Hata hivyo, mara nydingi huwa hawana ujuzi muhimu wa maisha na hawana mahali popote pa kwenda.

Hali hii huwfanya wawe katika hatari ya unyonyaji, biashara haramu na uraibu wa madawa ya kulevy. Baadhi yao hawana vitambulisho. Jambo hili linawazuia kupata makazi, ajira, matibabu au msaada wa kisheria, na hawawezi kupiga kura wakifikisha umri unaokubaliwa. Wengi wao hujihusisha na uhalifu au ukahaba, au hujipata wakiishi mitaani.

### KUWATETEA WASIOWEZA KUJITETA

Shirika la Mwanzo\* ndilo lililokuwa la kwanza katika Nchi za Asia ya Kati kushughulikia maswala ambayo yanawakabili vijana hawa. Kwa ushirikiano wa karibu na makanisa ya eneo hilo, wao huwasaidia vijana kuijunga tena na jamii. Wao huwapatia ushauri, mafunzo, ushauri wa kazi na msaada wa kisheria. Pia, wao huwapa makao ya muda hadi vijana hawa wanapopata mahali pengine pa kuishi.

Lakini shirika la Mwanzo halikutaka kutibu dalili za tatizo pekee. Waliamua kushawishi serikali na kutetea haki za vijana hawa (angalia kisanduku kilicho kando).

Kwanza, serikali ilikuwa inawashuku na ilikataa kusikiliza. Lakini katika kipindi cha miaka sita, shirika la Mwanzo lilijitahidi na kujenga uhusiano mzuri na serikali ya mitaa na ya kitaifa. Kustahimili kwao hatimaye kukazaa matunda. Katika mwaka wa 2016, walipewa jukumu la kusaidia kubuni sheria mpya za kulinda haki za watoto wakiondoka makao ya mayatima.

### KUHIMIZA FAMILIA ZA KULEA

Shirika lingine, Mabadiliko\*, huwa na kituo cha mgogoro kwa ajili ya watoto walio katika mazingira magumu. Kituo hiki huwatunza watoto kwa muda kabla hawajarudi nyumbani au kuijunga na familia za kulea. Shirika la Mabadiliko lilipoanza kazi yake, familia za kulea ilikuwa dhana mpya katika Nchi za Asia ya Kati. Watu wengi walihoji kile walichokifanya. Lakini shirika la Mabadiliko ilikuwa na malengo bayana. Walitamani sana kuona kila mtoto ambaye hangeweza kuishi na familia yake halisi, akipata nafasi katika familia za kulea. Walijua kwamba serikali yao ilikuwa imetia saini mkatuba wa Umoja wa Mataifa juu ya Haki za Mtoto (tazama ukurasa wa 3), hivyo ingwezekana kwao kuunga mkono sheria mpya ya kitaifa.

Walipata mafanikio wakati mfanyakazi wa kijamii alipatia shirika la Mabadiliko nafasi ya kuwasiliana na wizara ya serikali ya taifa, inayohusika na masuala ya watoto na familia. Baada ya hapo shirika la Mabadiliko lilishirikiana na mashirika mengine yaliyokuwa yanashughulikia suala la kulea. Kwa pamoja, wao walishawishi wizara hiyo hadi sheria ya kitaifa ilioongoza masuala yote ya kulea watoto ikapitishwa.

Sasa wanatekeleza sheria hiyo kwa kuhakikisha watoto katika mji wao, daima wanapata familia inayowafaa. Kila familia ya kulea hupata mafunzo, msaada unaoendelea na posho ya kifedha kwa kila mtoto.



Familia nydingi katika Nchi za Asia ya Kati zinaishi katika hali ya msingi sana.  
Picha: Alice Keen / Tearfund

# NJIA BUNIFU ZA KUWASHAWISHI WAFANYA MAAMUZI

## Kishawishi ni nini?

Dhana ya kushawishi inaweza kueleweka kama 'kuwasiliana moja kwa moja na wafanya maamuzi'. Lengo lake kuu ni kuwashawishi wabunge kuleta mabadiliko katika sheria, sera na mazoea.

Kushawishi kunajumuisha:

- Kuandika barua
- Kupiga simu
- Kupanga ziara au mukutano
- Kufanya ziara au mukutano
- Kumpangia mfanya maamuzi ziara ya kutembelea na kukutana na jumuiya iliyoathiriwa na suala husika.

## Kutumia uigaji kwa ubunifu: mfano

Wafanyakazi wa Mwanzo\* waliulizwa wawasilishe kesi yao mbele ya wabunge. Wakaandamana na vijana kadhaa kutoka vituo vya watoto. Kwa pamoja, wao waliigiza na kuiga kwa ufanisi:

- Kila waziri wa serikali alipewa kadi. Kila kadi ilikuwa imeandikwa kisa cha kawaida ambacho huenda kijana akakumbana nacho baada ya kuondoka makao ya mayatima.
- Mawaziri hawa walitakiwa kuchenza sehemu ya vijana hawa wakati wa kuigiza.

- Vijana nao walicheza sehemu ya viongozi wa mitaa (matibabu, makazi, ajira nk).

- Mawaziri walizungumza na 'viongozi wa mitaa' na 'walikatazwa kufikia' nyingi ya huduma walizoomba. Baadhi ya sababu zilizowafanya wakatazwe ni pamoja na kuwa na rekodi ya uhalifu au kutokuwa na pesa, elimu, hati za utambulisho nk.

Walipofika mwisho wa shughuli hii ya kuigiza na kuiga, mawaziri walikuwa wameguswa sana na hali yao. Waliunda kikundi cha kufanya kazi kilichopewa wajibu wa kuangalia tatizo hilo kwa kina.

Kwa sababu ya hili, katika kipindi cha zaidi ya miaka kumi iliyopita, hakuna mtoto hata mmoja kutoka mji huo ambaye amejipata katika makao ya mayatima.

## KUTETEA FAMILIA

Kwa ushirikiano na makanisa yaliyo karibu, shirika la Mabadiliko pia hufanya kazi na familia zilizopitia mazingira magumu ili kujaribu kuzuia kuvunjikia kwa familia hizi. Wao hupeana huduma za ushauri nasaha na mafunzo ya kiufundi, hivyo kuimarisha familia.

Utetezi katika ngazi ya mitaa ni sehemu muhimu ya kazi ambayo shirika la Mabadiliko linafanya kwa pamoja na familia. Wao huzisaidia familia kupata nakala mpya za hati walizopoteza kama vile vitambulisho na hati za mali. Pia huandika barua kwa mamlaka za mitaa kwa niaba ya watoto ambao wamekatazwa kupata elimu. Tatizo hili linaweza kutokea wakati watoto hawana hati sahihi za utambulisho, elimu ya chekechea, sare au viatu. Pia linaweza kutokea kwa sababu ya ubaguzi dhidi ya familia masikini. Wakati mwingine barua hizi zinaleta mafanikio na mamlaka za mitaa huhakikisha kwamba shule zinakubali watoto hawa waliopitia mazingira magumu.

Mashirika ya Serikali sasa hushirikiana na shirika la Mabadiliko wanapopata watoto waliopitia mazingira magumu. Wao huona shirika hili lina weledi na ni la kuaminika.

## MAMBO MSINGI YA KUJIFUNZA

**Tumia kanuni za Biblia.** Mashirika ya Mwanzo na Mabadiliko yanahamasishwa na kanuni ya kibiblia ya, 'Jifunze kufanya mema; tafuta haki. Tetea walokandamizwa. Watetee watoto yatima; watetee walio wajane "(Isaya 1:17). Hamu yao ya kushiriki upendo wa Mungu na watu walio katika mazingira magumu zaidi huwapa motisha wa kuendelea, hata wakati wanapingwa.

**Shirikisha kanisa lililo karibu.** Kufanya hivi huongeza pakubwa matokeo ya mashirika madogo. Katika Nchi za Asia ya Kati, familia nyingi za Kikristo huwalea watoto walipitia mazingira magumu. Washiriki wa kanisa huwafundisha watoto walio katika vituo kwa muda ujuzi mpya kama vile kupika na kushona. Pia hutoa msaada wa wachungaji na ushauri nasaha. Wanasheria kutoka kanisa hutoa msaada wa muda na utaalamu bila malipo ili kusaidia kurejesha hati za utambulisho na kutetea haki za watoto.

**Vumilia!** Ilichukua mashirika ya Mwanzo na Mabadiliko miaka mingi kushawishi serikali na mashirika mengine kwamba kulikuwa na tatizo, na pia kwamba walikuwa na makini kutafuta suluhisho. Hatimaye, juhudii na uaminifu wao ulizaa matunda. Sasa wanaweza kushawishi shughuli ya kubuni sheria zinazohusiana na watoto waliopitia mazingira magumu, katika ngazi za mitaa na kitaifa, na wanaweza kusaidia kuhakikisha kuwa sheria hizi zinatumika.



## MAPENDEKEZO YA JINSI YA KUTUMIA MAKALA HAYA

- Katika kikundi, jadili sera ambazo wafanya maamuzi katika eneo lako na katika taifa wamebuni kuhusiana na kutunza mayatima. Je, unakubaliana na sera hizo?
- Unaweza kutumia mawazo yoyote katika makala haya kushawishi wafanya maamuzi kuhusu haki za mayatima?

Tembelea [www.tearfund.org/advocacy\\_toolkit](http://www.tearfund.org/advocacy_toolkit) upate rasilimali za uhamasishaji, bila malipo.

*Jude Collins ni Afisa wa Habari za Mradi katika shirika la Tearfund. Hapo awali alijihusisha na maendeleo ya jamii huko Nepal na Honduras.*

Barua pepe: [jude.collins@tearfund.org](mailto:jude.collins@tearfund.org)

\*Majina yamebadilishwa.



## KUSAIDIA MAYATIMA KATIKA JAMII

Tulifurahia kusikia kuwa mnachapisha toleo la jarida la *Hatua kwa Hatua* linalojadili suala la utunzaji wa mayatima. Kuna 'mayatima wengi katika jamii' nchini Ufilipino ambao wametelekezwa au kutupwa na wazazi wao. Baadhi ni waathiriwa wa umaskini uliokithiri, majanga ya asili au vita. Wakati mwagine, watoto tuliofanya kazi nao wameishia mitaani hata baada ya sisi kutia jithada zetu zote. Jambo hili huvunja moyo na kukatisha tamaa. Wafanyakazi wetu wa jamii wangelia wakati wa maombi ofisini juu ya watoto kama hawa.

Watoto zaidi wamo katika hatari ya kuwa yatima katika jamii kutokana na hatari kubwa ya majanga nchini Ufilipino. Tunataraja shirika la Tearfund linaweza kutupa zana halisi za jinsi ya kushughulikia suala hili kwa njia uendelevu.

**LINGAP (MSHIRIKA WA TEAR UHOLANZI)**



## TATIZO NGUMU

**Swali: 'Ikiwa makao ya mayatima yanaendeshwa kama familia, bado yanaweza kusababisha matatizo kwa watoto?'**

**Jibu:** Baadhi ya makao ya mayatima hujaribu kutoa huduma 'inayolingana na familia'. Wanaweza kutunza idadi ndogo tu ya watoto. Au wanaweza kuweka watoto katika "vikundi vya familia", ambapo wanatunzwa na mlezi katika boma ndogo ndani ya makao hayo. Ingawa mwelekeo huu ni bora kuliko taasisi kubwa, bado hauweki kujaza pengo la familia.

Hata makazi madogo ya yatima yanayoiga mfano wa familia hubadilisha wafanyakazi na yana sheria na ratiba nyinyi zaidi ya familia. Makao ya mayatima yanayoipanga katika boma ndogo ndani ya makao yale bado hujitengenezea jumuiya yao wenye. Huwa hayaweki mtoto katika jumuiya halisi



## KUPAMBANA NA UNYANYAPAA DHIDI YA WATOTO

Toleo la 86 la jarida la *Hatua kwa Hatua* lilojadili unyanyapaa lisaidia sana kijiji changu. Tulikuwa na watoto viziwi, bubu, viwete na wenye VVU, pamoja na wasichana wawili wadogo ambaao walikuwa karibu kubakwa. Watoto hawa walikuwa wakidhihakiwa na hawakuweza kwenda shulen na kucheza na marafiki zao. Hata wazazi wao waliwfungia nyumbani, kwa kuogopa aibu.

Nilitembelea watoto hawa kwa usaidizi wa kamati za wakuu wa kijiji. Tulizungumza na wazazi na walezi wao kuhusu vile Yesu alivyowapenda watoto, viwete, vipofu na kila mtu. Baada ya miezi miwili ya kuwashawishi, waliruhusu watoto wao waanze kutagusana na marafiki zao. Pia tulizungumza na marafiki zao na kuwaambia wafikirie kama ingekuwa wao katika hali ile na jinsi ambavyo wangehisi. Kisha tukaanza shule ya kijiji na klubu ya michezo. Baada ya kusikia kuhusu upendo, watu walibadilisha mtazamo na tabia zao kuhusiana na mayatima, watoto wenye ulemavu na waliopitia mazingira magumu.

**SAMSON, ZAMBIA**

na jamii pana. Jambo hili litaathiri watoto watakapoondoka makao yale. Makao ya mayatima hutunza idadi kubwa ya watoto kadri muda unavyopita. Hawawezi kuwa wazazi kwa watoto wote katika kila hatua ya maisha yao.

Madhara ya kukua katika taasisi yanaweza kupunguzwa kuitopia mazingira yanayolingana na familia, lakini huenda yasiondolewe. Kwa hiyo, ingawa kuwa katika makao yanayoiga familia ni bora kuliko kuwa katika taasisi kubwa, chaguo bora zaidi ni kutunzwa na famili au jamii, ikiwa inawezekana.

*Jibu lilitolewa kwenye hati ya shirika la ACCI Kinnectedy ya Maswali Yanayoulizwa Sana.*

*Je, una tatizo ngumu ambalo ungependa jumuiya ya Hatua kwa Hatua ikusaidie kutatua? Wasiliana nasi kuitopia anwani iliyo hapo chini.*

## HATUA KWA HATUA

*Hatua kwa Hatua* ni jarida linalouganisha wafanyakazi wa afya na maendeleo duniani kote. Ni njia ya kuwatia moyo Wakristo wa mataifa yote wanapofanya kazi kwa pamoja ili kujenga ustawi katika jamii zao.

Jarida la *Hatua kwa Hatua* hupatikana bila malipo kwa wafanyakazi wa maendeleo mashinani na viongozi wa kanisa. Wale ambao wana uwewe wa kulipa wanaweza kujisajili kwa kuwasiliana na Mhariri. Kufanya hivi hutuwezesha kuendelea kuwapa wanaohitaji sana, nakala bila malipo.

Wasomaji wanaalikwa kuchangia maoni, makala, barua na picha.

Jarida la *Hatua kwa Hatua* pia linapatikana katika Kifaransa kama *Pas à Pas*, katika Kireno kama *Passo a Passo* na katika Kihispania kama *Paso a Paso*. Aidha, linapatikana katika Kihindi.

Mhariri Zoe Burden

Tearfund, 100 Church Road, Teddington, TW11 8QE, UK

Simu: +44 20 8977 9144

Faksi: +44 20 8943 3594

Barua pepe: publications@tearfund.org

Tovuti: www.learn.tearfund.org

Mhariri Tafsiri Helen Machin

Shukrani za kipekee kwa Markus Köker na Tearfund Ireland. Shirika la Tearfund Ireland limetupa ushauri wa kiufundi na msaada wa kifedha katika kuandaa toleo hili.

Kamatii ya uhariri: Barbara Almond, Mike Clifford, Jude Collins, Steve Collins, Paul Dean, Helen Gaw, Alice Keen, Ted Lankester, Melissa Lawson, Liu Liu, Roland Lubett, Ildephonse Nzabahimana, Amos Oumounabidji, Naomi Sosa, Shannon Thomson, Rebecca Weaver-Boyes, Joy Wright

Kusanifu: Wingfinger Graphics, Leeds

Mifano isipokuwa wakati parmeleewza vinginevyo, mifano imetoka kwa Petra Röhr-Rouendaal, *Ambapo hakuna msanii* (toleo la pilii)

Limechapishwa kwenye karatasi inayotumiwa tena iliyoidhinishwa na FSC, kwa kutumia mbinu zisizothiri mazingira.

Kujisajili: Andika barua au utume barua pepe, na utoe maelezo mapufi ya kazi yako na uchague lugha unayoipendelea, kwa kutumia anwani zilizotolewa hapo juu. Vinginevyo, fuata maagizo yaliyo hapo chini ili ujandikishe kupokea toleo pe la *Hatua kwa Hatua* na uchague kupokea nakala zilizochapishwa.

Toleo pepe la Jarida la *Hatua kwa Hatua* ili kupokea nakala ya jarida hili kuitopia barua pepe, tafadhalii jiandikishe kwenye tovuti ya Tearfund Learn (hapo juu). Fuata kuungo cha 'jiandikishe upokee nakala ya jarida la *Hatua kwa Hatua*' kwenye ukurasa wa nyumbani.

Mabadiliko ya anwani Tafadhalii tupe nambari ya kurejelea kutoka lebo ya anwani yako wakati unatuulishwa kuhusu mabadiliko ya anwani.

Hakimiliki © Tearfund 2017. Haki zote zimehidhifi. Yeyote ana ruhusa ya kutumia maandishi kutoka jarida la *Hatua kwa Hatua* kwa madhumuni ya mafunzo, lakini lazima awe amelipata jarida hili bila malipo na atambulishi Tearfund kama chanzo. Kwa matumizi mengine yoyote, tafadhalii wasiliana na publications@tearfund.org ili kupata ruhusa ilioandikwa.

Maoni yoyote yaliyoandikwa kwenye barua na makala si lazima yawe yanaambatana na yale ya mhariri au Tearfund. Taarifa za kiufundi zilizotolewa katika jarida la *Hatua kwa Hatua* zimechunguzwa kwa kina kadiri iwezekanavyo, lakini hatuwezi kukubali uwajibikaji ikiwa kuna matatizo yoyote.

Tearfund ni shirika la Kikristo la misaada na maendeleo linalosaidia kujenga mtandao wa kimatifa wa makanisa katika maeneo mbalimbali, ili kusaidia kutokomeza umasikini.

Limechapishwa na Tearfund. Kampuni iliyowekwa kikomo kuitopia dhamana. Iemesajili wa nchini Uingereza Nambari 994339.

Shirika la Misaada la Usajili Nambari 265464 (Uingereza na Wales)

Shirika la Misaada Usajili Nambari SC037624 (Uskoti)

# HAKUNA MTOTO ANAYEACHWA NYUMA

*Watoto wenyewe ulemavu ni miongoni mwa wenyewe uwerekano mkubwa wa kuwekwa katika makao ya mayatima. Wazazi wengi hawajui jinsi ya kumtunza mtoto mwenye ulemavu na mara nyingi jamii haisaidii sana. Shirika la Care for Children linabadilisha hali hii kwa watoto wenyewe ulemavu nchini Uchina na kupata matokeo ya ajabu.*

Mnamo mwaka wa 1998, serikali ya Uchina iliuliza mwanzilishi wa Care for Children, Robert Glover, aanzishe mradi wa majaribio wa kuwahamisha watoto kutoka makao ya mayatima na kuwaweka katika familia. Kwa kushirikiana na Tearfund, Robert alihamia Shanghai akiwa na familia yake. Wakati huo hakukuwa hata na neno la kuelezea 'huduma ya kulea' katika lugha rasmi ya Uchina, Mandarin (sawa na hadithi ya Casa Viva katika ukurasa wa 18). Lakini katika kipindi cha miaka mitatu, watoto 500 walikuwa wamewekwa katika familia zilizo kwenye eneo hilo.

Miaka kumi na nane baadaye, shirika la Care for Children limesaidia watoto laki tatu (300,000) kuhamia katika nyumba za familia zinazowapenda. Shirika hili sasa linafanya kazi nchini Thailand, na litaanza shughuli zake nchini Vietnam na Malaysia katika 2017. Maono ya shirika hili ni kuhamisha watoto milioni 1 kutoka taasisi na kuwaweka katika familia.

Robert anatoa sababu kadhaa kwa nini watu nchini Uchina wana hamu ya kutoa huduma za muda mrefu za kulea watoto:

- Katika Uchina, familia na jamii ni muhimu sana. Hadi hivi majuzi, serikali ya Uchina ilikuwa na sera iliyoruhusu kila familia kupata mtoto mmoja tu, hivyo wanandoa wengi waliruhusiwa kuzaa mtoto mmoja peke yake (ingawa kulikuwa na vighairi). Hata hivyo, wazazi wanataka kutunza watoto zaidi.
- Familia nyingi za kulea ni Wakristo na wanahamasishwa na imani yao ya kuonyesha upendo kwa wale wanaouhitaji.
- Serikali ya Uchina imesaidia kueneza ujumbe kuhusu kutunza mtoto akiwa katika familia. Wao huzitambua familia zinazokubali kumlea mtoto kwa kuweka bango nje ya nyumba zao.

## KULEA WATOTO WENYE ULEMAVU

Shirika la Care for Children husaidia kutafutia watoto wote familia mpya, wale walio na ulemavu na wale hawana. Watu wengi wanadhani ni vigumu sana kwa watoto wenyewe ulemavu kupata familia za kulea. Lakini kulingana na uzoefu wetu katika Care for Children, familia nyingi nchini Uchina na Thailand wako tayari kulea watoto wenyewe ulemavu. Hili linatokana na mfano wa Care for Children na msaada maalum ambao wanapatia familia za watoto wenyewe ulemavu.



Long Xiao alizaliwa na kaakaa lilopasuka na wazazi wake halisi wakamtupa. Lakini kupitia usaizidi kutoka shirika la Care for Children, sasa ana familia mpya ya kulea ambayo inampenda na kumtia moyo.

Picha: Care for Children

Watoto wanapoondoka kwenye makao ya mayatima na kuijunga na familia, shirika la Care for Children husaidia taasisi kubadilisha mkakati na kuwa kituo cha usaizidi kwa jamii. Baadhi ya mabadiliko haya ni kama mipango ya kusaidia watoto wenyewe mahitaji maalum, kama kutoa huduma za tibamaungo. Shirika la Care for Children huwapa wafanyakazi katika makao haya ya mayatima mafunzo ya kuwawezesha kusaidia jamii, na wao hupewa familia 20 za kushughulikia. Jambo hili hurahisishia familia za kulea jukumu la kutunza mtoto mwenye ulemavu.

.....

Shukrani kwa Robert Glover. Ili kutazama video ya kazi ya shirika la Care for Children, tembelea <http://youtu.be/r5Q-AmcrHag>

Tovuti: [www.careforchildren.com](http://www.careforchildren.com)  
Barua pepe: [info@careforchildren.com](mailto:info@careforchildren.com)



## UCHUNGUZI KIFANI: KIJINI CHA AJABU KARIBU NA KUNMING

*Yang Jia ni kijiji kidogo katika milima karibu na Kunming, Uchina. Kinaweza kuonekana kama kijiji cha kawaida – lakini kimefanya jambo la ajabu. Familia hamsini na tatu katika jamii hii hizmechukua watoto 166 kutoka kwa makao ya mayatima yaliyo karibu. Zaidi ya asilimia 90 ya watoto hawa wana ulemavu mkali wa kiakili au kimwili.*

'Huu ni mradi wa kipekee sana,' anasema Sun Yuan Jie, Msimamizi wa Miradi huko Uchina katika shirika la Care for Children. 'Watu hapa

huwapa watoto hawa moyo. Wao huwapenda watoto hawa na kusaidiana wenye.' '

Kwanza, shirika la Care for Children lilitembelea makao ya mayatima huko Kunming, na kuwafundisha wazazi na kuwaandaa watoto. Baada ya watoto kuijunga na familia zao mpya, wafanyakazi walikuwa wamepewa mafunzo na Care for Children walishughulikia suala la ufuatiliaji na kutoa msaada.

'Bila shaka kuna changamoto,' anasema baba mmoja wa kulea kutoka Yang Jia. 'Lakini

tunakabiliana nazo. Furaha tunayopata huzidi changamoto.' Watoto wanapopata upendo na utunzaji kutoka kwa familia zao mpya, wao huanza kustawi na kutabasamu tena.

'Sisi tunawapenda sana,' mama mmoja wa kulea anaongeza. 'Tunawapenda kama kwamba ni watoto wetu, na wao wanatupenda kama kwamba sisi ni wazazi wao.'

Wazazi huko Yang Jia wanasema kwamba wakati walipata furaha zaidi katika miaka kumi iliopita, ilikuwa waliposikia watoto wakiwaita 'mama' na 'baba' kwa mara ya kwanza.